


UKURASA 3

## HAKIMU awa mkali kusuasua upelelezi kesi ya Ole Sabaya


Nipashe
TESA
Jumanne Agosti 30, 2022
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Fahamu namna ya kupunguza kero, migogoro kwenye familia

Ukurasa 12

Kasi ya wanafunzi kunaswa mtego mimba utotoni inatisha

Ukurasa 13

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

Moto wa nyika ulivyo maangamizi kwa wanyama, mimea na kitisho cha utalii

MOTO wa nyika ni moto unaowaka bila kupangwa na wakati mwingine usiodhibitiwa wala usiochagua pakuwakia, unaweza kulipuka popote iwe mijini au vijijini.

Hivi karibuni mataifa ya Ulaya yakiwa kwenye kiangazi kilichoambatana na joto kali linalozidi nyuzi 42 kwa mfano nchini Uingereza zilipata pia changamoto ya moto wa nyika.

Nchi za Romania, Austria, Ujerumani, Ureno na Afrika Kaskazini na mataifa ya Algeria na Tunisia ni miongoni mwa maeneo yaliyotishiwa na moto wa nyika uliosababishwa na joto hilo kwenye ukanda wa Mediterranean.

Moto wa nyika ni habari zinazosikika kwa kasi hasa miezi ya hivi karibuni.

Swala 'oryx' na miti ya 'erica arborea' bayoanuai inayopatikana Mlima Kilimanjaro pekee. PICHA ZOTE:MTANDAO

UKURASA 11

Jumanne Agosti 30, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581053

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Askari polisi asimulia alivyochomwa mshale

UKURASA 2



Muuguzi Kiongozi Wodi ya Upasuaji ya Hospitali ya Benjamin Mkapa, Sawia Arabi, akimhudumia askari polisi William Werema wa Kituo cha Polisi Mrijo, Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma, aliyelazwa hospitalini hapo kwa kudaiwa kuchomwa mshale na Nanda Songo mkazi wa kijiji cha Chioli wilayani humo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

UKURASA WA 2

### UKUSANYAJI MAONI KIKOSI KAZI WAELEKEA UKINGONI

UKUSANYAJI wa maoni ya wadau wa demokrasia na siasa nchini, unaelekea ukingoni...

UKURASA WA 4

### WAZIRI UMMY AHADHARISHA KUWAPO KIPINDUPINDU

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ametahadharisha...

UKURASA WA 4

### UFUNGAJI 'LUKU' MITA ZA MAJI WAFIKIA 30%

SERIKALI imesema ufungaji wa mita za maji katika mfumo wa kulipia kabla ya kutumia huduma hiyo...

UKURASA WA 5

### MWINYI AHIMIZA UMUHIMU BIMA ILI KULETA MAGEUZI YA KIUCHUMI

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema malengo ya nchi na jumuiya mbalimbali katika...

## Serikali yaongeza siku saba zaidi sensa

UKURASA 3

# Samia adhamiria uteuzi majaji kufikia 50 kwa 50



UKURASA 2




Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (katikati), akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa mashine ya kwanza ya kubadilishia fedha (FX ATM) ya Benki ya NMB katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna na wa pili kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa KIA, Christine Mwakatobe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**MICHEZO** SIMBA YAPEWA FAILI LA BIG BULLETS CAF UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Mitsubishi, Yasuteru Hirai, katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa TICAD uliofanyika jijini Tunis, Tunisia, juzi. Waziri Majaliwa ameiomba kampuni hiyo kujenga kiwanda cha kuunganisha magari Tanzania. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Ukusanyaji maoni kikosi kazi waelekea ukingoni

**Na Jenifer Gilla**

UKUSANYAJI wa maoni ya wadau wa demokrasia na siasa nchini, unaelekea ukingoni baada ya Kikosi Kazi cha Kukusanya Maoni ya Wadau wa Demokrasia ya Vyama vya Siasa nchini, kikimaliza kazi hiyo mjini Pemba.

Mwenyekiti wa Kikosi Kazi hicho, Prof. Rwekaza Mukandala, aliiambia Nipashe kuwa jana walikutana na kukusanya maoni kwa wadau zaidi ya 70 katika mji wa Chakechake mkoani Pemba Kaskazini na leo watamalizia mjini Wete. Aliyataja makundi yaliyotoa maoni hayo kuwa ni vyama vya siasa, mashirika yasiyo ya kiserikali, viongozi wa dini, watu mashuhuri, wanawake na vijana.

"Tukishamaliza huku tutakutana Unguja kwa ajili ya kuandika ripoti ya jumla kwa kuzingatia hoja zilizojitokeza mara nyingi zaidi kwa huku Zanzibar na Tanzania Bara kisha tutampelekea Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) mapendekezo tuliopokea," alisema Mukandala.

Alisema ukusanyaji wa maoni hayo pia unafanyika kwa njia ya maandishi kupitia barua pepe, ujumbe wa WhatsApp au kuwasilisha moja kwa moja katika Ofisi za Msajili wa Vyama vya Siasa zilizoko Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar.

Akizungumza na chombo cha habari mapema mwezi huu, Makamu Mwenyekiti wa Kikosi hicho, Hamad Rashid, alisema kuwa mchakato huo ulisimama kwa muda kwa sababu mbalimbali zikiwamo kupisha matukio ya kitaifa huku viongozi wengi wa juu wa Zanzibar wakiwa Tanzania Bara na kusababisha jitihada za kujitokeza kutoa maoni yao kuwa ngumu.

Kikosi kazi hicho kiliundwa na Rais Samia mwaka jana, muda mfupi baada ya kuanza majukumu yake ya kazi ya urais, kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake ya kufanya kazi kwa pamoja na vyama vya upinzani ili kuweka mazingira ya usawa katika siasa na kuheshimu demokrasia.

# Askari polisi asimulia alivyochomwa mshale

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

ASKARI polisi wa Kituo cha Mrijo wilayani Chemba mkoani Dodoma, Konstebo William Werema, ameeleza alivyonusurika kifo baada ya kushambuliwa kwa mshale unaodhaniwa kuwa na sumu alipokuwa akitekeleza majukumu yake.

Werema alijeruhiwa juzi na mkazi wa kijiji cha Chioli wilayani humo, Nada Songo, baada ya kudaiwa kuwatishia makarani wa sensa kwa mishale akigoma kuhesabiwa.

Akizungumza jana katika Hospitali ya Benjamini Mkapa jijini hapo, alikolazwa kwa matibabu, askari huyo alisema alikuwa akijaribu kumkamata mtuhumiwa huyo baada ya kupokea taarifa kuwa anahatarisha amani ya wananchi wa kijiji hicho pamoja na makarani wa sensa.

"Ilikuwa Agosti 28, tulipata taarifa kwa wananchi kuwa kijijini kwao kuna mtu anatishia watu kwa mishale ikipita kwenda kwenye ng'ombe pamoja na watoto wanaopita. Sisi Jeshi la Polisi tuliokabidhiwa kulinda usalama wa raia na mali zao tulifika ili kuwasaidia wananchi hao," alisema.

Werema alisema walipofika nyumbani kwake wakiwa wameongozana na ndugu zake, hawakumkuta mtuhumiwa na wakaelezwa kuwa anatembea na mishale.

Alisema wakiwa nje ya nyumba yake, ghafla walimwona mtuhumiwa akitoka kwenye kichaka kilicho jirani na nyumbani kwake na kumwamrisha ajisalimishe kwa amani lakini alianza kurusha mishale mfululizo na ndipo mshale mmoja ukampata tumboni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo katika kitongoji cha Manyata kijijini hapo huku akisema askari huyo alichomwa mshale unaodhaniwa kuwa wa sumu na mtuhumiwa Nanda Songo (45) ambaye alifariki dunia kutokana na kujeruhiwa na risasi maeneo ya kifuani na mguu wa kulia alizopigwa wakati akiwashambulia askari kutokana na kukaidi kukamatwa.

Pia alisema mtuhumiwa huyo alimjeruhi askari wa jeshi la akiba (mgambo) Juma Madodo kwa mshale mguu wa kulia ambaye amelazwa hospitalini kwa matibabu.

Alibainisha kuwa mtuhumiwa alikutwa na mishale 23, pinde mbili, visu viwili, ala ya kuwekea mishale, dawa mbalimbali za kienyeji na hati ya kumaliza kifungo katika gereza la King'ang'a wilayani Kondoa. Alikuwa mfungwa namba 46/2022 kuanzia Agosti 13, 2021 hadi Februari 11, mwaka huu.

**ALIGOMA KUHESABIWA**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Chioli, Sadick Ndalu, alisema hakuwapo wakati wa tukio lakini alijulishwa na mtendaji wa kijiji kuwa mtuhumiwa aliwatishia kwa mishale makarani wa sensa na viongozi walipofika nyumbani kwake kutaka kumhesabu.

"Agosti 27, mwaka huu, makarani walifika lakini walipotishiwa ilitolewa taarifa ndipo polisi walipokuja hawakumkukuta na kurudi jana (juzi) wakakutana na kadhia hiyo," alisema. Ndalu alisema wakati askari wakimtafuta ndani ya nyumba yake alijitokeza kutoka kwenye kichaka cha jirani alipojificha na kuanza kuwashambulia askari kwa mishale.

Pia alisema mtuhumiwa aliwahi kuwashambulia watu wawili kwa mishale, kuua baadhi ya mifugo ya watu pamoja na kumshambulia kwa kisu dada yake wa kuzaliwa tumbo moja.

# Samia adhamiria uteuzi wa majaji 50 kwa 50

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema uteuzi wa idadi kubwa ya majaji wanawake alioufanya kwa kipindi cha miezi 17 toka aingie madarakani, umesaidia kupunguza malalamiko ya wananchi kwa mhimili wa mahakama nchini.

Aidha, amesema ili kumaliza malalamiko yote yanayotolewa dhidi ya mhimili huo, anapanga uteuzi wa majaji wanawake na wanaume kufikia asilimia 50 kwa 50.

Samia, alisema hayo jana Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma, baada ya kuwaapisha majaji 21 wa Mahakama Kuu na Kamishna Jenerali wa Magereza, Mzee Nyamka.

Alisema, katika kipindi cha miezi 17, ameteua majaji 43 wa Mahakama Kuu na wengine tisa wa Mahakama ya Rufani wakiwamo wanawake 23.

"Kama alivyosema awali Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, kuwa hadi sasa idadi ya majaji wanawake ni kama asilimia 37 lakini lengo langu huko mbele ni kuwa na wastani wa 50 kwa 50. Hata hawa 21 ambao nimewaapisha leo (jana), wanawake ni 10 na wanaume 12.

"Malalamiko dhidi ya mhimili huu yaliyokuwa yakitolewa hapo awali hivi sasa yamepungua sana. Hii yote ni kutokana na utawala bora chini ya Jaji Mkuu, Tume ya Utumishi wa Mahakama, maboresho mbalimbali yaliyofanywa, weledi lakini kuongeza idadi kubwa ya majaji wanawake kumesaidia sana kuondoa malalamiko," alisema.

Rais, alisema pamoja na majaji wanawake na wanaume kusoma kozi zinazofanana bado kuna kitu tofauti kwao katika utoaji wa hukumu.

"Hukumu za jaji mwanamume huwezi kuzikuta kabisa kwa jaji mwanamke kwa kuwa anapohukumu kama ni mtoto anamwangalia kama mama lakini mwanamume anaweza kuletwa mtu kapigwa kachakaa anamuuliza wewe kabila gani anasema Mkurya, anasema ninyi si ndiyo mambo yenu?" Alisema.

Samia pia, aliwataka majaji wanawake ambao wamepata nafasi hiyo kufanya kazi kwa kuzingatia kiapo chao na sheria za nchi.

"Wanawake nimewapa nafasi nawaombeni msiniangushe. Mnapokaa kwenye kiti ninyi ni majaji si wanawake," alisema huku akisisitiza kuwa ataendelea kufanya uteuzi kwa mujibu wa katiba na sheria na uchumi utakavyoruhusu.

**JAJI MKUU ASHUKURU**

Jaji Mkuu Prof. Juma alimshukuru Rais Samia, kwa kuendelea kuteua majaji wengi hali ambayo itapunguza mrundikano wa mashauri.

"Mheshimiwa Rais tunakushukuru sana huu kwetu sisi mahakama ni uwezeshaji mkubwa sana kwani hadi sasa umeteua na kuwaapisha majaji 52 wakiwamo 43 wa Mahakama Kuu na tisa wa Mahakama ya Rufani na hawa ambao wamekula kiapo leo wanakwenda kupunguza mzigo wa kesi 300 kwa kila jaji uliokuwapo awali. Sasa hawa 21 wa leo (jana) wanakwenda kufanya wastani kupungua hadi kufikia kesi 265 kwa jaji mmoja," alisema.

**MAAGIZO MAZITO**

Katika hatua nyingine, Rais Samia alimtaka Kamishna Jenerali wa Magereza (CGP) Mzee Nyamka, kwenda kuzifanyia kazi changamoto zote zilizoko katika taasisi hiyo.

"Nakupongeza sana kwa nafasi hii kwani nilikuwa na majina matano lakini la kwako ndilo lilikidhi viwango, hivyo nakutake uende kufanyia kazi tatizo la utawala bora ambalo hivi sasa halipo kabisa katika taasisi hii. Peleka watu mafunzo kwani kuna watu toka mafunzo ya mwisho hawajawahi kupata muda huo tena," alisema.

Rais alimwagiza pia kwenda kusimamia utawala wa haki ndani ya jeshi hilo pamoja na kufanya kazi ya msingi ya kurekebisha wafungwa.

"Tumekuwa tunatoa misamaha kwa wafungwa lakini unakuta kesho wanarudi tena. Inabidi sasa kwenda kufanya kazi ya kurekebisha watu ili akitoka asirudie tena na awe na kitu cha kufanya.

"Lakini kwenye Shirika la Uzalishaji Mali, kasimamie matumizi ya fedha na uhakikishe fedha zote zinakwenda katika magereza yote nchini," aliagiza.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema anaendelea kutekeleza maelekezo ya Rais ili kuboresha utendaji wa Jeshi la Magereza ikiwamo marekebisho ya baadhi ya kanuni.

"Mheshimiwa Rais ulituagiza kuona ni jinsi gani jeshi hili linafanya kazi zake za msingi bila kuchanganya masuala ya biashara. Kwa kuanza tumefanya marekebisho kwa shirika la uzalishaji mali. Katibu wake mtendaji atakuwa mtu mwingine na si Kamishna Jenerali wa Magereza kama ilivyokuwa awali," alisema.

HABARI KITAIFA

# Hakimu awa mkali kusuasua upelelezi kesi ya Ole Sabaya

**Na Mwandishi Wetu,**
MOSHI

HAKIMU Mkazi Mwandamizi, Salome Mshasha, anayesikiliza kesi ya uhujumu uchumi na rushwa inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake wanne, jana alikuwa mkali kuhusu kuchelewa kukamilika kwa upelelezi.

Kutokana na hali hiyo, alitaka kazi hiyo ikamilishwe ili kutoa haki kwa washtakiwa kujua hatima ya shauri lao.

Kabla ya kuahirisha kesi hiyo Na. 2 ya mwaka 2022 iliyoko katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, Mshasha alisema upande wa mashtaka katika kesi hiyo una wajibu wa kukamilisha upelelezi huo badala ya kila siku washtakiwa kupelekwa mahakamani bila kujua haki yao na mwisho wa kesi hiyo.

Wengine wanaokabiliwa na kesi hiyo ni Sylvester Nyegu, John Aweyo, Nathan Msuya na Antero Assey.

"Upande wa mashtaka, hoja zinazoendelea kutolewa na upande wa utetezi zinahitaji majibu. Si kila siku washtakiwa wanakuja mahakamani na majibu ni yale yale. Wana haki ya kujua hatima yao katika kesi hii. Labda tutakapokuja Septemba 12, tutajua tumefikia wapi," alisema na kuahirisha shauri hilo hadi tarehe hiyo litakapotajwa tena.

Wakili wa Utetezi, Hellena Mahuna, alidai mahakamani kuwa bado wana malalamiko yale yale ya kutaka upande wa mashtaka kukamilisha upelelezi pamoja na kupatikana kwa kibali cha kusikiliza kesi hiyo.

"Mheshimiwa Hakimu, tarehe 1/6/2022 Wakili wa Serikali Mwandamizi aliomba siku tano ili alete kibali lakini mpaka sasa hatujui nini kimetokea. Ni vyema wakamilishe upelelezi, walete kibali na ikiwezekana tufanye committal hapa (kikao cha kufungasha ushahidi kwenda Mahakama Kuu) ili twende Mahakama Kuu," alidai.

Alipomaliza kutoa hoja hiyo, Wakili wa Serikali Sabitina Mcharo, alisimama na kujibu kuwa: "Tunayafanyia kazi malalamiko haya na upelelezi utakamilika mheshimiwa."

Ole Sabaya na wenzake wanakabiliwa na mashtaka saba likiwamo la kuongoza genge la uhalifu katika wilaya ya Hai, Februari 2, mwaka jana.

Shtaka la pili la rushwa, linamkabili mshtakiwa wa kwanza, Ole Sabaya, anayedaiwa kulifanya Februari 22, mwaka jana, kwa kuomba rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Godbless Swai katika eneo la Bomang'ombe wilayani Hai.

Shtaka la tatu, Ole Sabaya anadaiwa kujipatia rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Elibariki Swai, kwa nia ya kuzuia taarifa ya uchunguzi zilizohusiana na ukwepaji wa kodi.

Aidha, shtaka la nne na la tano, linawakabili mshtakiwa wa pili, watatu, wa nne na wa tano, ambalo ni kumsaidia mstakiwa wa kwanza (Ole Sabaya) kushawishi na kujipatia manufaa asiyostahili ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Alex Swai, huku wakijua ni kinyume cha sheria.

Shitaka la sita, linamkabili Ole Sabaya, ambalo ni ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma katika wilaya ya Hai wakati na shtaka la saba ni utakatishaji wa fedha, ambalo linawakabili washtakiwa wote.

# NBS yaongeza siku 7 kukamilisha sensa

**Na Waandishi Wetu**

KAMISAA wa Sensa, Anne Makinda, amesema Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), imeongeza siku saba kukamilisha Sensa ya Watu na Makazi huku waliohesabiwa hadi jana saa 2:00 asubuhi wakifikia asilimia 93.45.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Makinda alisema siku hizo zimeongezwa ili kuwafikia Watanzania wote na kufanya sensa ya majengo ambayo itaanza leo.

Makinda alisema katika taarifa zilizokusanywa, wamebaini kuwa bado kuna asilimia 6.5 ya kaya ambazo hazijahesabiwa ndiyo maana wametoa muda hadi Septemba 5, mwaka huu ili kaya hizo zifikiwe.

Pia, Makinda alisema wataanza mchakato wa kuhesabu makazi ambao utaendeshwa kwa siku tatu, huku akitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa makarani, ili suala hilo likamilike kama inavyotarajiwa.

"Waratibu wa sensa katika wilaya wamefanya utaratibu wa kuongeza makarani kutoka maeneo ya jirani, wamekamilisha kuhesabu kwenda kwenye maeneo yenye uhitaji ili kazi hiyo ikamilike kwa wakati," alisema.

"Endapo itatokea hujahesabiwa leo (jana) bado unayo nafasi ya kuhesabiwa na katika kufanikisha hili, NBS imetoa namba maalumu kwa ajili ya wananchi ambao hawajahesabiwa kupiga simu makao makuu ili utaratibu wa kupeleka karani eneo husika ufanyike kwa wakati, namba hiyo ni 0753665491," aliongeza.

Makinda, ambaye pia ni Spika Mstaafu wa Bunge la Tanzania, alitoa wito kwa wananchi ambao hawajahesabiwa kwenda ofisi za serikali za mitaa na kumwachia mwenyekiti au mtendaji namba za mawasiliano ili makarani wawafikie walipo na kuhesabiwa.

Pia, aliwasihi wananchi kutumia namba hiyo kwa lengo la kufanikisha sensa na siyo vinginevyo, huku akiendelea kusisitiza kamati za sensa ngazi za mkoa, wilaya, kata, vijiji na mitaa kuhakikisha wanatoa namba za mawasiliano kwa ajili ya wananchi ambao watakuwa hawajahesabiwa, ili kupiga simu kueleza waliko ili waweze kufikiwa.

Makinda pia, alisema sensa ya makazi itajumuisha kukusanya taarifa ya majengo yote ya makazi na yasiyo ya makazi nchi nzima, kwaajili ya kuboresha sera na kupanga mipango ya kimkakati ya kuboresha sekta ya nyumba nchini.

"Napenda kutoa wito kwa wananchi wote kuendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa makarani waliowahesabu katika maeneo yenu kwa kutoa taarifa sahihi za majengo, makarani waliofanya sensa ndio hao hao watapita kwenye majengo yote yaliyopo kwenye maeneo ya kuhesabia watu ili kukusanya taarifa za majengo," alisema Anna.

**Imeandikwa na Maulid Mmbaga (DAR), Fatuma Athumani, Owen Bariki na Sabina Ntobi (TUDARCo)**


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA UTOAJI WA SHUGHULI ZA UMEME NA UFUNGAJI MITAMBO PAMOJA NA KAZI ZA AWALI ZA KUKABIDHI**

**KUMB ETJ-BB-PE-EI-MEP-SI-001-00**

BESIX Ballast Nedam Limited, inatekeleza maandalizi ya awali ya ujenzi wa Gati na Kituo cha kupakia mafuta ghafi katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao :

**Shughuli za Umeme na Ufungaji mitambo pamoja na kazi za awali za kukabidhi (Pre-Commissioning).**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Meli za Mafuta, Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**
- Ufungaji wa njia na vishikio vya nyaya, mfumo wa kuzuia radi na mitetemo ya ardhini, Mfumo wa Taa
- Ufungaji wa nyaya za umeme mkubwa, umeme mdogo na mawasiliano (MV, LV na ELV cables)
- Ufungaji wa vifaa na mitambo eneo la kazi
- Kuchomelea na kusimika mabomba yenye kipenyo cha 30" yaliyosakinishwa awali kwenye yadi ya utengenezaji pamoja na uwekaji wa vitanzi vya upanuzi vya kipenyo cha 30"
- Ufungaji wa kipande cha bomba (Spool Piece) cha 20"
- Ufungaji wa bomba la 4" na chini ya ukubwa wa CS ikijumuisha vihimili na vali
- Kapaka Rangi maalumu, mabomba na Vali, kuzuia kutu au uharibifu
- Ufungaji wa bomba la GRE kwa kuunganisha
- Kupasha joto bomba baada ya kuchomelea
- Huduma za NDT za kuchomelea bomba
- Ufungaji wa mfumo wa usalama eneo la kazi na vifaa vya zima moto
- Ufungaji wa chuma na mihili
- Ununuzi wa vifaa vya matumizi na zana muhimu za ujenzi.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zenye nia, zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuambatanisha yafuatayo:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali kutekeleza kandarasi husika,
- Orodha ya uzoefu iliyo na historia ya ugavi / rekodi safi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika kutekeleza huduma na kazi husika kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au kazi zinazofanana.
- Orodha ya mafundi chuma na uchomeleaji (welders) wenye utaalamu na waliothibishwa
- Sera ya Ubora ya Kampuni na mipango ya afya, usalama na mazingira sehemu za kazi pamoja na vyeti vya uthibitisho,
- Viwango vya ubora vya kimataifa: ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018), EN ISO 14732, EN ISO 90606-1, ISO 11484, EN ISO 90609-1, EN ISO 90609-1 cheti cha EN ISO 10801 equi 1, 10891 au EN ISO 10808 equi 1, 10891, EN ISO 90609-1 au vinavyofanana.
- Kuzingatia kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP), unapendekezwa zaidi.

Makampuni yenye nia ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati husika kwa **procurement@bbnjv.com** . **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe 1**4 Septemba 2022, 12:00 Mchana Saa za Tanzania.**

Makampuni yanayokidhi vigezo yatatathminiwa na yakichaguliwa, yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zitakazo pita mchujo wa awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

2170195O1




# Ummy ahadharisha kuwapo kipindupindu

Na Halfani Chusi

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ametahadharisha kuwapo mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu katika baadhi ya mikoa na kuwataka Watanzania kuzingatia usafi wa mazingira, maji na chakula, ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Ummy aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa semina ya mafunzo yaliyoandaliwa na Shirika La Afya Dunia (WHO), kuijengea uwezo serikali na wadau mbalimbali katika kupambana na ugonjwa wa kipindupindu.

Alisema serikali inatambua kuwapo kwa ugonjwa huo na kutaka kila mtu kuzingatia usafi wa maji na vyakula ili kukabiliana nao.

"Tanzania kuna jumla ya wagonjwa 519 wenye ugonjwa wa kipindupindu kati yao 11 wameshafariki dunia, gonjwa hili limeshamiri zaidi katika mikoa ya Rukwa Kigoma na Katavi kuanzia Agosti 3 hadi 27, mwaka huu," alisema na kuongeza:

"Wamegundulika wagonjwa 39 kutoka Mkoa wa Katavi Wilaya ya Tanganyika kwa hiyo kipekee tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwekeza fedha nyingi na nguvu kubwa katika upatikanaji wa majisafi na salama katika maeneo mbalimbali."

Alisema ugonjwa huo unaenezwa kupitia chakula na kutumia maji yasiyo salama, lakini kinachoshtua kila watu 100 wanaokufa 30 ni waafrika.

"Tumekubaliana na mimi nitawahamasisha washiriki wa semina hii kwamba tunao wajibu wa kutimiza wajibu wetu, ili kuepukana na gonjwa hili hatari kwa kuhakikisha tunawagundua wagonjwa mapema, kuimarisha mifumo ya afya pamoja na kujiandaa na njia za kukabiliana na magonjwa ya mlipuko."

Aliwaagiza wakuu wa wilaya nchini kuweka vipaumbele kwenye kudhibiti kipindupindu pamoja na kuzitaka halmashauri kutunga sheria ndogo ndogo zitakazo saidia kudhibiti majitaka.

"Dar es Salaam hapa kuna watu wana tabia ya kusubiri mvua ikinyesha wanafungulia bomba la maji machafu, tabia hii haikubaliki lazima tuweke adhabu kali ukimwambia mtu ametiririsha maji machafu halafu alipe faini Sh. 10,000 ni ndogo sana inatakiwa faini iwe kubwa zaidi ya gharama ya kukodi gari la maji machafu sasa mtanzania apime mwenyewe alipe faini kubwa au aite gari la majitaka," alisema.

Vile vile, alisema usimamizi wa taka za majumbani haufanyi vizuri na kwamba wananchi wapo tayari kulipia uzoaji, lakini wahusika hawafanyi kazi kwa moyo na weledi na kutoa mfano kuwa gari la taka linaweza lisipite kwa siku mbili.

Naibu Waziri wa Maji, Injinia Maryprisca Mahundi, alisema serikali inaendelea kuwekeza nguvu kubwa kwenye upatikanaji wa majisafi na salama ili kusaidia wananchi kujiepusha na magonjwa ya mlipuko yanayosababishwa na maji.

"Hakikisha maji unayonawa yanakwenda chini au kwenye chombo ambacho huwezi tena kuyatumia tuache ule utamaduni wa zamani kila mmoja anawe maji yake kwa sabuni, tukumbuke kuosha matunda kwa majisafi na salama," alisema.

Mratibu wa Mradi huo kutoka WHO, Zabroni Yot, alisema wameamua kuleta mafunzo hayo baada ya kubaini uwapo wa waathirika wa ugonjwa huo akibainisha kuwa mafunzo hayo yatasaidia jamii kufahamu njia za kujikinga na kumaliza vifo vitokanavyo na magonjwa ya mlipuko ifikapo 2030.

Mafunzo hayo yameshafanyika katika nchi nne za Afrika ikiwamo Angola, Malawi, Msumbiji, Zambia Tanzania, ikiwa nchi ya tano kupata mafunzo hayo.



Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mpwapwa jijini Dodoma, Rev. George Chiteto (aliyelala), akiwekwa wakfu kuwa askofu wa kanisa hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ufungaji 'LUKU' mita za maji wafikia 30%

Na Halfani Chusi

SERIKALI imesema ufungaji wa mita za maji katika mfumo wa kulipia kabla ya kutumia huduma hiyo, umefikia asilimia 30 kwa nchi nzima.

Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira kutoka Wizara ya Maji, Joyce Msiru, alisema hayo jana Dar es Salaam alipozungumza na Nipashe huku akibainisha kuwa baadhi ya kaya zimeshafikiwa na huduma hiyo.

Alisema azma ya serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 kila kaya kuwa imefikiwa na huduma hiyo huku akiwaomba Watanzania kuwa na subira kwani mradi huo unahitaji gharama na muda kukamilika.

Kukamilika kwa mradi huo, alisema kutasaidia mambo mengi ikiwamo kupunguza migogoro ya maji katika nyumba za kupanga na kwa watumiaji wenye miradi mikubwa.

"Mradi wa ufungaji mita hizo unaendelea katika baadhi ya mikoa. Mpaka sasa umefikia asilimia 30, hivyo niwatoe hofu Watanzania kwamba mradi huo utakamilika kwa sababu unahitaji gharama kubwa," alisema.

Alifafanua, kuwa mfumo huo utakuwa unamtaka mtumiaji kulipia maji kabla ya kuanza kuyatumia kama ilivyo kwenye mita za umeme.

"Lengo la serikali ni kuona watu hawagombani kwa ajili ya bili za maji kwa hiyo mfumo huu utasaidia kutibu malalamiko ya wateja, pia utasaidia kudhibiti mianya kwa wale waliokuwa wanajipatia maji kwa njia za panya, utasaidia kumfanya mteja alipe bili yake kwa wakati pamoja na kusaidia kukusanya mapato ya serikali kwa urahisi," alisema Msiru. Alisema, hakuna gharama yoyote anayopaswa kulipia mwananchi ili kupata huduma hiyo, akibainisha kuwa kwa mikoa ambayo imeshaanza kufaidika na huduma hiyo wafuate utaratibu ili kufikiwa.

"Katika mikoa ambayo huduma hii imefika tumeanza kufunga kwenye miradi mikubwa baada ya hapo ndio tutaingia kwenye kaya moja baada ya nyingine na katika ufungaji huo mwananchi hatalipia chochote," alisema.

Septemba, mwaka jana, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso aliagiza mchakato wa kufunga mita za maji za Luku uende haraka, ili kuondoa malalamiko ya ubambikiaji wa bili za ankara za maji nchini.

Aweso alisema kutokana na malalamiko kutoka kwa wateja, hivi sasa wameamua kuja na mita za maji za Luku.

## Wananchi, viongozi waridhika na sensa

Na Waandishi Wetu

WANANCHI wa maeneo mbalimbali mkoani Dar es Salaam, wameridhika na sensa ya watu na makazi ilivyofanyika, huku baadhi wakisubiri kuhesabiwa.

Nipashe ilitembelea maeneo mbalimbali mkoani Dar es Salaam kwa viongozi wa mitaa kuelezea kwa kiasi gani kuna mafanikio ya wananchi wengi kuhesabiwa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mbezi Juu, Rehema Muyo, alisema kwenye eneo lake wamewafikia wananchi kwa asilimia 99 na wako watu ambao walikataa kuhesabiwa walielimishwa na baadaye walikubali.

"Mimi nashukuru kwenye mtaa wangu watu wote wamehesabiwa na kwa waliogoma tunawazoa na kuwaleta ofisini kwa ajili ya kupewa elimu na wanakubali na kurudi majumbani kwao kwa ajili ya kuhesabiwa," alisema.

Mjumbe wa Mtaa wa Mlalakuwa, Kata ya Makongo wilayani Kinondoni, Rehema Komba, alisema kwenye mtaa wake hawajapata malalamiko ya wananchi ambao hawajahesabiwa.

Karani Mkuu wa Mtaa wa Mlalakuwa, Sophia Kawawa, alisema kazi imefanyika vizuri na kwamba vifaa vilivyotumika kwenye kazi hiyo viko salama. Huku mjumbe wa Mtaa wa Mwenge, Twaha Stamili, akisema: "Changamoto kwenye makanisa makarani walikuwa hawajui kama wachungaji wanaishi ndani, lakini wajumbe tulihakikisha wanafikiwa kwa ajili ya kuhesabiwa."

Mwenyekiti wa Mtaa wa Bwawani Kata ya Kijitonyama wilayani Kinondoni, Felisianus Kamkala, alisema katika eneo lake sensa imefanyika vizuri.

Naye Jimmy Mgaya, mkazi wa mtaa wa Bwawani alisema makarani washapita katika kaya yake na ameshahesabiwa, hivyo anasubiri serikali itoe takwimu za idadi ya watu katika nchi.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Mbezi Kati Kata ya Mbezi Juu, Jofre Mlaponi, alisema sensa imefanyika vizuri kwenye mtaa wake licha ya baadhi ya vijana kukataa kuhesabiwa lakini baadaye walivyoelimishwa walikubali kujibu maswali waliyoulizwa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nzasa, Kata ya Makongo wilayani Kinondoni, Edward Mfanga, alisema mchakato umekamilika kwa asilimia kubwa na kuwapongeza wananchi kwa ushirikiano.

**Imeandikwa na Joram Gervas, Isiyaka Nyamihasi, Camila Bonanza, Victoria Mgodomi (TUDARCo), Saumu Hassani (DSJ), Beatrice Mwaigomole (SAUT) na AISHA KONDO (DSJ)**



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akihutubia wakati wa kufungua Mkutano Mkuu wa 44 wa Umoja wa Wanabima Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika, uliowashirikisha wadau wa Bima, katika ukumbi wa Hoteli ya Madinat Al Bahr Mbweni Wilaya ya Mjini Unguja, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi ahimiza umuhimu bima ili kuleta mageuzi ya kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema malengo ya nchi na jumuiya mbalimbali katika kuleta mageuzi ya kiuchumi, yanapaswa kwenda sambamba na upangaji na utekelezaji wa mipango ya kuimarisha huduma za bima kwa misingi kuwa wawekezaji huzingatia sana jambo hilo.

Dk. Mwinyi alisema hayo jana katika Mkutano Mkuu wa 44 wa Umoja wa Wanabima katika Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika (OESAI), uliofanyika katika Hoteli ya Madinat Al Bahr Mbweni, Mjini Magharibi.

Alisema, uwapo wa huduma bora za bima na zenye uhakika katika nchi wanachama wa OESAI, ni miongoni mwa mambo ya msingi yanayozingatiwa na wawekezaji pale wanapofanya uamuzi wa kuwekeza katika miradi ya maendeleo.

Alisema Kaulimbiu ya mkutano huo isemayo "Kuimarisha Sekta ya Bima kwa Maendeleo Yajayo' inaendana na azma ya nchi nyingi barani Afrika zinazopitia katika mageuzi makubwa ya kiuchumi, kupanua wigo katika sekta za uzalishaji na kuendeleza sekta mpya ambazo hazikuwapo kabla.

Dk. Mwinyi alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha sekta ya bima ili kuweka kinga kwa ajili ya mitaji mikubwa wakati huu huduma za uchimbaji madini barani Afrika zikiimarika, uchimbaji wa mafuta na gesi, uendelezaji wa viwanda pamoja na kupanda kwa kiwango cha ubunifu katika sayansi na teknolojia.

"Nchi nyingi za Visiwa hivi sasa zimeweka mkazo katika kuendeleza uchumi wa bluu ambao umeweka mkazo shughuli zinazohusu matumizi bora ya rasilimali za bahari, huku nchi nyingine zikiwa zinakuza sekta za usafirishaji, kilimo, uvuvi pamoja na ufugaji", alisema.

Zanzibar, alisema ikiwa nchi ya visiwa, imeweka mkazo katika kuimarisha uchumi wa bluu katika mwelekeo wake wa kiuchumi, ambapo zamani ilitegemea zaidi sekta ya kilimo, husuan cha karafuu, na kubainisha mahitaji ya huduma za bima ambazo zinapaswa kubadilika ili kuendana na mabadiliko hayo.

Pia, alisema serikali ya Tanzania imejikita kuwekeza katika sekta ya nishati ya mafuta na gesi, ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji pamoja na viwanja vya ndege, bandari na barabara, hivyo akabainisha umuhimu wa mashirika ya bima kuunga mkono hatua hiyo ili kutoa kinga kwa wawekezaji na wadau.

Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi, alisema juhudi za kuleta mageuzi ya kiuchumi barani Afrika zinakumbana na changamoto nyingi,ikiwamo ukosefu wa mitaji, hususan rasilimali fedha.

Alisema, hivi sasa kumekuwapo ugumu na ushindani mkubwa wa kupata mitaji kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo inayolengwa kutekelezwa.

Alitumia fursa hiyo kuyahimiza mashirika na taasisi za bima barani Afrika kuwa na utayari na ubunifu wa kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo katika nchi zao badala ya kukaa na kusubiri kutoa huduma za bima pekee.

Katika nchi zilizoendelea, alisema mashirika ya bima, mifuko ya hifadhi ya jamii na taasisi za fedha imekuwa na mchango mkubwa katika upatikanaji wa fedha na mitaji ili kutekeleza miradi kradi ya maendeleo pamoja na kukuza ajira.

Alizishauri taasisi za fedha kuondokana na utaratibu wa kubaki na fedha wakati mahitaji ya fedha hizo yapo na makubwa, na hivyo akazitaka kujifunza katika Taasisi za nchi zilizoendelea ili kuona kwa namna gani fedha zinaweza kutumika kwa miradi ya mendeleo.

Rais Dk. Mwinyi aliyahimiza mashirika ya bima kuendelea na juhudi za kutanua huduma zake na kuyafikia makundi mbalimbali ya wajasiriamali, wakulima, wavuvi pamoja na wafugaji walioko vijijini.

Akizungumzia utekelezaji wa malengo ya Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA), Dk. Mwinyi alisema mkazo mkubwa umewekwa ili kukuza biashara na shughuli za Ujasiriamali Barani Afrika.

Dk. Mwinyi alisema ufanisi na mzunguko wa wafanyabiashara, bidhaa, huduma na mahitaji kati ya nchi na nchi Barani Afrika, unahitaji kuwepo kwa huduma za Bima zilizo imara kwa kiwango cha Kikanda na Kimataifa.

## Tanzania yawasilisha miradi minane TICAD

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali ya Tanzania imewasilisha miradi minane yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 1.334 katika Mkutano wa Nane wa Kimataifa wa Wakuu wa Nchi na Serikali unaohusu ushirikiano wa maendeleo baina ya Japan na Afrika (TICAD) ambao ulimalizika jana.

Miradi iliyowasilishwa ni ya ukarabati wa barabara ya Morogoro-Dodoma kwa kiwango cha lami, umwagiliaji katika Bonde la Ziwa Victoria, kusambaza maji Lugoda (Mufindi), kujenga uwezo wa kituo cha utafiti cha ufugaji wa samaki Dar es Salaam, bandari ya kisasa ya uvuvi, kuanzisha maabara ya kuthibitisha ubora kwenye sekta ya uvuvi na ukarabati wa bandari ya uvuvi ya Wete na ujenzi wa njia ya umeme ya Somanga-Fungu-Mkuranga.

Akizungumza jana jijini Tunis, Tunisia, ambako alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mkutano huo, Waziri Mkuu alisema alipata fursa ya kuwaeleza washiriki wa mkutano na nchi ya Japan juu ya utekelezaji wa miradi yake kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

"Kupitia mikutano ya TICAD, sisi tumenufaika na ujenzi wa daraja la Mfugale, mradi wa kufua umeme wa Kinyerezi II na sasa tumeomba watukamilishie miradi mitatu ya barabara ya Arusha-Holili, Bandari ya Kigoma na mradi wa maji wa Zanzibar," alisema Majaliwa kama alivyokaririwa na taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu jana.

Alisema miradi mitatu ambayo imeombewa fedha inahitaji dola za Marekani milioni 343.8 na kati ya hizo, dola milioni 221 ni kwa ajili ya mradi wa barabara ya Arusha - Holili, dola milioni 98.7 za mradi wa kuboresha miundombinu ya usambazaji wa maji Zanzibar) na dola milioni 24.1 kwa bandari ya Kigoma.

Kuhusu kilimo, Waziri Mkuu alisema kupitia TICAD, Tanzania imeomba kupewa kipaumbele ili kuongeza wigo wa sekta hiyo ili kuhakikisha kunakuwa na chakula cha kutosha pamoja na ziada kwa ajili ya kuuza nje.

Waziri Mkuu pia alifanya mikutano na viongozi wa kampuni za Japan Tobacco Incorporation (JTI), Mitsubishi na Rais wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA).

Majaliwa alimshukuru Mwenyekiti wa Bodi ya JTI, Mutsuo Iwai, kwa kuamua kujenga shule ya bweni ya wasichana wilayani Urambo na akaomba kuendelea kununua zaidi tumbaku kutoka kwa wakulima.

"Mwaka jana walinunua tani milioni 14 kwa hiyo tumewaomba msimu huu waongeze tani zaidi ili kuwapa uhakika wa soko wakulima wetu. Wao wana kiwanda kwa hiyo wanaweza kununua zaidi," alisema.

Waziri Mkuu pia alimshukuru Makamu wa Rais wa Mitsubishi, Yasuteru Hirai, kwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umeme mkoani Kilimanjaro na akaomba waangalie uwekezekano wa kuwekeza kwenye sekta ya kilimo na hasa kwenye uzalishaji wa mbolea.

"Eneo tunalolihitaji sana ni uzalishaji wa mbolea. Kama walivyofanya Asia kwa kuzalisha tani milioni 1.2, tumewaomba waje nchini kwa sababu mahitaji yetu ni makubwa. Pia tumewashawishi waje kujenga kiwanda cha kuunganisha magari hapa nchini badala ya kuagiza kutoka kwao," alisema.

Naye Rais wa JICA, Dk. Akihiko Tanaka, alimwahidi Waziri Mkuu kuwa wafanyakazi wa kujitolea waliokuwa wakifanya kazi nchini lakini wakalazimika kurudi Japan kwa sababu ya UVIKO-19 wataanza kurudi hivi karibuni ili waendelee kutoa huduma nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Majaji wanawake waonyeshe kuwa wanaweza kwa vitendo

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, jana aliwaapisha majaji 21 wa Mahakama Kuu ya Tanzania aliowateua hivi karibuni ili kuongeza kasi ya utendaji na ufanisi wa mhimili huo wa dola ambao umekuwa ukilalamikiwa kwa kuchelewesha mashauri, hivyo wananchi kukosa haki pamoja na kutumia gharama kubwa hadi kumalizika.

Uteuzi wa majaji hao ni mwendelezo wa kuhakikisha mhimili huo unafanya kazi zake kwa weledi na pia majaji kupunguziwa mzigo wa kesi ambazo zimerundikana kwa muda mrefu. Tangu aingie madarakani miezi 17 iliyopita, Rais ameteua majaji 43 hatua ambayo imeongeza ufanisi katika Mahakama Kuu na ile ya rufani ambayo ni ya juu kabisa katika kutafsiri sheria na kutoa uamuzi katika kesi mbalimbali za jinai na madai.

Miongoni mwa majaji walioteuliwa na Rais wamo wanawake 23. Hatua hiyo imemwezesha mhimili wa Mahakama kufikisha asilimia 37 ya majaji wanawake, hivyo kuifanya Tanzania kupiga hatua katika azma ya kufikia usawa wa kijinsia wa asilimia 50 kwa 50 kwa mujibu wa makubaliano na mikataba mbalimbali ya kimataifa kuhusu usawa wa kijinsia kwenye ngazi za uamuzi, zikiwamo za siasa, uongozi na utendaji kitaasisi.

Katika hafla hiyo, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alibainisha kwamba ongezeko la majaji katika ngazi hizo, limepunguza malalamiko yaliyokuwa yakitolewa dhidi ya mhimili huo.

Kwa hatua hiyo, Rais anastahili pongezi katika uteuzi mbalimbali anaoufanya, si kwa majaji tu bali hata kwa viongozi wa wizara na taasisi mbalimbali za serikali wakiwamo mawaziri na manaibu wao, wakuu wa mikoa, wilaya na makatibu tawala wa mikoa na wilaya. Kila anapoteua, kumekuwa na idadi ya kuridhisha ya wanawake lengo likiwa kuelekea usawa wa 50 kwa hamsini wa kijinsia kwenye ngazi za uamuzi.

Pamoja na kuteuliwa wanawake wengi, suala hapa si kuangalia idadi pekee bali utendaji wenye viwango na weledi vinatakiwa ili kumhakikishia Rais kwamba hakufanya makosa kuwateua katika nafasi hizo. Msemo kwamba wanawake wakiwezeshwa wanaweza, udhihirike katika utendaji wenye kasi, viwango na weledi.

Katika miaka kadhaa iliyopita, kuliibuka malalamiko kuwa baadhi ya majaji wanaoteuliwa, wakiwamo wanawake, walikuwa hawaandiki huku hatua iliyosababisha wananchi waliokuwa na mashauri mahakamani kukosa haki.


Licha ya kulalamikiwa kuhusu kutoandika hukumu kwa mwaka mmoja au zaidi, pia kulikuwa na tuhuma za rushwa dhidi ya baadhi ya majaji kuwa walikuwa wakiandika hukumu mbili katika kesi moja kuangalia nani atatoa dau kubwa ili ampendelee kwa kumpa ushindi. Ni vyema majaji wapya wanawake wanapoanza kazi hiyo yenye heshima kubwa katika jamii, ni vyema wakazingatia viapo vyao na kufanya kazi kwa misingi ya kitaaluma bila kuwa na upendeleo wala huba kwa upande wowote kwenye kesi husika. Kwa maneno mengine, wanatakiwa kufuata misingi ya sheria na taratibu zinazowaongoza katika kusikiliza hoja zinazotolewa na hatimaye kutoa hukumu stahili.

Ni dhahiri kwamba kwa kufanya hivyo, wataonyesha imani kubwa kwa wananchi pamoja na Rais ambaye amewaamini kushika nyadhifa hizo pamoja na vyombo vilivyofanya uchunguzi hadi kupatikana kwao kwamba wanafaa kuwa majaji. Ni wazi kwamba kulikuwa na majina mengi yaliyopendekezwa kuwa majaji na hatimaye kupatikana watu 21 ambao Rais aliridhia na kuwateua.

Mbali na kufanya kazi kwa weledi, majaji hao wanawake wanapaswa kufuata miiko na desturi kwa ajili ya kuonyesha kwamba nafasi hizo ni za heshima, hivyo kila wanalofanya mahali popote, kikazi au maisha binafsi, waonyeshe heshima na nidhamu ya hali ya juu.

Mwisho, majaji hao wanawake wanapaswa kuonyesha kuwa Rais hakuwapendelea katika kuwateua, hivyo waonyeshe uwezo katika majukumu yao mapya ili aendelee kuwa na imani nao na hatimaye kuteua wanawake zaidi. Kwa mantiki hiyo, wasimwangushe Rais bali waonyeshe kuwa wanaweza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanahitaji kuchunguzwa akili kwa kuzika aliyehai

Na Halfani Chusi

**HILI** halivumiliki. Ndivyo unavyoweza kusema, ukirejea tukio la wananchi wanaojidai wana hasira kali pamoja na baadhi ya wanafamilia huko mkoani Ruvuma kumwadhibu hukumu ya kifo Mzee John Komba (78), kwa kumzika akiwa hai, kwa madai ya kuhusishwa na mauaji ya mwanawe Severine Komba (34).

Uhalifu huo ulitokea katika Kijiji cha Mahanje wilayani Madaba, jambo lililosababisha wazee wengine mkoani humo kuishi kwa wasiwasi na mashaka makubwa ya kuuliwa , kama vile si watu wanaostahili kuwapo dunia.

Huu naweza kusema ni zaidi ya unyama, kukatisha uhai wa mtu kwa kusingizia mambo ambayo hayana uhakika, lakini hata kama ni ukweli sheria haimruhusu mtu yeyote kuzikwa akiwa hai au kuzika mwenzake akiwa hai. Wala kuhukumu kuwa ni muuaji bila kufikishwa mahakamani.

Ni siku kadhaa zimepita tangu mzee Komba afariki dunia kwa kukuzikwa hai akisababishiwa kifo na watu wanaoamini ushirikina na ambao huenda hawana imani za dini zinazokataza kuua na tena kumtendea ubaya binadamu mwenzao.

Kupitia tukio hilo Baraza la Wazee la Taifa (BWZT), pamoja na mtandao wa mashirika yanayotetea haki za wazee nchini kama HelpAge International Tanzania, wamejitosa kukemea unyama huo.

Mwenyekiti wa Baraza, Lameck Sendo, anasema tukio hilo ni mwendelezo wa matukio ya kinyama wanayofanyiwa wazee kutokanana na imani potofu ya dhana za kishirikina.

"Tumepokea kwa masikitiko tukio la mauaji ya Mzee John Komba, aliyeuliwa kwa kuzikwa akiwa hai katika Kijiji cha Mahanje, kitendo hicho inasemekana kimefanywa na baadhi ya wananchi na wanafamilia yake, wakati wakiwa kwenye mazishi ya mtoto wake Severine Komba, wakimtuhumu mzee huyo kuwa alihusika katika mauaji ya mwanaye. Hili limeshangaza na kusikitisha."

Anasema, mkasa huo unawakumbusha tukio jingine kama hilo lililotokea mkoani Singida, katika Kijiji cha Kisharita wilayani Iramba, ambako wazee watatu wanawake waliuawa siku moja kwa kutuhumiwa kwa uchawi, mambo ambayo hayawezi kuthibitika.

Kitendo alichofanyiwa John Komba, ni kuvunja sheria za nchi, katiba pamoja na kwenda kinyume na imani za dini kwa hiyo ifike mahali watu watambue kuwa uzee ni hatua katika ukuaji ambayo ni muhimu, hata watoto, vijana na yeyote ataifikia hivyo wawaheshimu hao waliozeeka.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu haikijanyamaza, ni jambo lisilovumilika, Mkurugenzi Mtendaji Anna Henga,anaeleza kuwa kitendo hicho hakikubaliki katika jamii na kuitaka serikali kuchukua hatua dhidi ya wa waliohusika kutoa hukumu ya kifo kwa mzee huyo, ambaye hana hatia.

Ni ombi la kila mmoja serikali ichukue hatua kali ambazo zitakuwa funzo kwa watu wengine ambao wanajihusiha na unyama huo, hii ni ajabu watu kumzika mtu akiwa hai, si jambo zuri mwenye jukumu la kukatisha uhai wa mtu ni aliyemuumba siyo wanakijiji au familia.

Sisi tunaomba serikali ifanye hima kukomesha tabia hiyo maana sasa inaota mizizi mtu akizeeka kidogo utasikia mchawi uzee upo hata ukiwa kijana ukifanikiwa kukaa kwa muda mrefu lazima utazeeka tena watu wanaomba kuishi na kuufikia uzee mwema, hivyo jambo hilo halikubaliki.

Jamii inapaswa kukumbuka kuwa wazee hawa ndiyo waliowalea wakiwa wadogo mpaka wamefikia umri wa kutambua baya na zuri sasa kama wanania mbaya si wangekatisha uhai wao tangu wakiwa wadogo kwa sababu kwa kipindi hicho ingekuwa raisi zaidi.

Jeshi la Polisi mkoani humo kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Songea akiwamo Mkuu wa Wilaya na kamati yake ya ulinzi na usalama, wanastahili pongezi kwa hatua za haraka walizozichukua ikiwamo kuwabaini na kuwakamata washtukiwa wa tukio hilo.

Ushauri wangu kwa wananchi ni vyema linapotokea tatizo kama hilo kutoa taarifa kwa polisi ili mtuhumiwa akamatwe na kuhojiwa itasaidia kubaini ukweli ulipo kuliko kujichukulia sheria mkononi kwa sababu unaweza kumuua mtu asiye na hatia kama ilivyokuwa kwa Mzee John Komba.

HABARI KITAIFA

## Ongezeko usafiri bodoboda hifadhini tishio

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKALA wa Uhifadhi wa Misitu nchini (TFS), umebaini ongezeko la usafiri wa bodaboda ndani ya hifadhi ya misitu kutishia uharibifu wa mazingira.

Pia, ucheleweshwaji wa uamuzi ya Kamati ya mawaziri wanane, iliyoteuliwa kushughulikia migogoro kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi umetajwa kuchangia ongezeko la wavamizi wa hifadhi.

Kamishna wa Uhifadhi, Prof. Dos Santos Silayo, alitoa kauli hiyo kwenye kikao cha kwanza cha TFS tangu ianzishwe kuwa Jeshi la Uhifadhi kilichofanyika jana jijini hapa.

Katika kikao hicho pia askari 479 walivalishwa vyeo vya madaraja mbalimbali.

Akizungumzia uharibifu wa mazingira unaosababishwa na pikipiki, Prof. Silayo alisema vyombo hivyo vya usafiri vinafanya kazi bila kufuata sheria za misitu na usalama barabarani katika hifadhi hiyo, jambo linalochangia kuwapo tishio la usalama wa hifadhi.

Alisema watu hao huvuna mazao ya misitu ikiwamo kubeba mkaa, kuni, kitendo kinachochangia uharibifu wa misitu katika maeneo mbalimbali na ukiukaji sheria ya misitu.

"Vyombo vya usafiri wa pikipiki umeongezeka katika maeneo ya hifadhi ya misitu na vingi vinafanyakazi bila kufuata sheria, tunaomba mamlaka husika kulifanyia kazi suala hilo ili kupunguza uharibifu," Prof. Silayo.

Alisema mikoa ya Kanda ya Kusini, Magharibi na Ziwa inakuwa na adha hiyo kutokana na matumizi makubwa ya nishati ya misitu, kwenye kilimo na uvunaji wa misitu na kuongeza kuwa ina uhitaji wa matumizi ya nishati ya misitu.

Kuhusu kuongezeka kwa wavamizi, alisema kunatokana na kucheleweshwa kwa uamuzi wa Kamati ya mawaziri na kutoa faida kwa wavamizi kuzidi kuongezeka katika maeneo mbalimbali ya misitu ya hifadhi nchini.

"Tunaomba suala hilo lishughulikiwe haraka ili tuweze kuendelea na taratibu na sheria za kuzuia uvamizi katika maeneo ya misitu," alisema Silayo.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, alitaka TFS kuendelea kubuni vivutio vitakavyozidi kushawishi na kuwavutia watalii ili kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan katika filamu ya Royal Tour ambayo imechangia kuongeza watalii hapa nchini.

# Bil. 100/- za gesi kupunguza makali mafuta

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amesema Sh. bilioni 100 zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya teknolojia ya gesi asilia zitasaidia kupunguza matumizi ya fedha nyingi zinazotumika katika mafuta.

Shaka aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipotembelea mradi wa kuunganisha mfumo wa gesi asili katika magari katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na kumpongeza Rais Samia kwa kuwekeza fedha hizo kwenye eneo hilo.

Alisema endapo fedha hizo zitasimamiwa vyema na waliopewa dhamana, matokeo yake yatakuwa makubwa na tija katika nchi.

"Kwa sasa tuko katika vita vya kiuchumi na hili ni thamani muhimu kwenye mapambano ya vita vya uchumi. Japo hili likisimamiwa vizuri, na waliopewa dhamana wakafanya kazi yao vizuri, matokeo yake ni makubwa na tija kwenye taifa letu. Kwanza, itapunguza matumizi makubwa ya mafuta kwenye magari yetu," alisema Shaka.

"Teknolojia hii itasaidia kwenye suala la usafirishaji endapo uhamasishaji utafanywa vizuri na wafanyabiashara wa ndani wakahamasishwa na serikali ikajipanga vizuri kwenye kujenga vituo vya kusambaza gesi," aliongeza.

Shaka alisema jambo la msingi ni kuwa na wataalamu wa kutosha ambao watasimamia kazi hiyo waliyoianza.

Alisema suala lingine ni kusaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana endapo mipango itawekwa ya kuwaandaa kwa kutumia fursa hiyo ambayo imeibuliwa na kuwatoa kwenye kilio cha ukosefu wa ajira kwa vijana.

"Huu utaratibu ukiwekwa kupitia mikoa na wilaya, DIT ikajitanua. Naamini tunaweza kuwasaidia vijana na Watanzania kutumia rasilimali hii ya gesi tuliyo nayo. Uchumi tunao ni lazima utumike vyema. Hii mipango itoke katika vichwa vyetu iende kufanya kazi ili fursa ziende kwa wengi," alisema Shaka.

Alisema serikali inapaswa kupongezwa na kuungwa mkono, kwamba teknolojia hiyo itawatoa katika utegemezi wa mafuta kama taifa.

Shaka alisema kumekuwa na jitihada mbalimbali zinazofanywa Rais Samia hasa kwenye uwekezaji wa fedha nyingi za maendeleo na kwamba wamepata fursa ya kutembelea na kuona namna wanavyotumia utaalamu wa kubadilisha miundombinu hiyo kutoka kwenye mafuta na kwenda katika gesi.

Alisema DIT imejitahidi kujitanua katika masula ya teknolojia na kusimamia kifungu cha 67 (c) cha Ilani ya Uchaguzi ya CCM, wanayotekeleza si matakwa yao ama utashi wao.

Mkuu wa DIT, Prof. Preksedius Ndomba, alisema kuna akiba ya futi trilioni 57.5 za gesi asilia ambayo imeifanya Tanzania kuwa nchi ya 82 duniani.

Alisema DIT itaendeleea kuwekeza katika vituo vya umahiri ili iweze kujitegemea na kushinda vita vya kiuchumi.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Kituo cha Gesi Asilia cha DIT, Dk. Esebi Nyari, kuhusu moja ya magari yanayofungwa mfumo wa kutumia gesi wakati wa ziara yake ya kutembelea mradi wa kufunga mfumo wa gesi (CNG), katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bunge laagiza kukamilishwa mchakato kupata mwendeshaji mpya mwendokasi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC), imeagiza kukamilishwa kwa mchakato wa kumpata mwendeshaji mpya wa Mradi wa Mabasi yaendayo kwa Haraka Dar es Salaam (DART).

Mradi huo kwa sasa unaendeshwa kwa mpito na kampuni ya Usafirishaji jijini Dar es Salaam (UDA) kupitia mradi wa usafirishaji wa UDART na Septemba, mwaka huu, serikali inatarajiwa kutia saini mkataba na kampuni kubwa kutoka Umoja wa Nchi za Kiarabu (UAE).

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jerry Silaa, alibainisha hayo jana baada ya kuchambua taarifa ya Wakala wa DART huo.

Alisema katika kikao hiko, DART imeahidi mwanzoni mwa Septemba, mwaka huu, watatia saini mkataba wa makubaliano na kampuni hiyo.

"Kikubwa kamati imeendelea kuwapongeza utakumbuka UDART ilipoanza ilikuwa na tiketi za mkono na baadaye ikaingia katika tiketi za kielektroniki. Kwa maelekezo ya serikali wameanza mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa tiketi ambao unamilikiwa sasa na serikali," alisema.

Silaa alibainisha kuwa hali hiyo imechangia mapato ya mradi huo kuongezeka kutoka Sh. bilioni 25 mwaka wa fedha 2020/21 hadi Sh. bilioni 36 mwaka 2021/22.

"Tumeelekeza DART kuendelea kusimamia mapato ya kielektroniki, kuboresha utendaji na kukamilisha mchakato wa kumpata mwendeshaji mpya na tumeagiza huyu UDART ambayo ni kampuni ya wazawa na inamilikiwa na serikali kumtengenezea mshindani. Ukimtengenezea mshindani wananchi watanufaika na ubora wa huduma, nauli na hata huduma wanazozipata zitakuwa zinaenda vizuri zaidi," alisema.

Pia alisema kwa sasa kampuni hiyo inaendesha vizuri awamu ya kwanza ya mradi huo ambayo ni kuanzia Kimara kwenda Posta wakati awamu ya pili ya Mbagala hadi Kariakoo ikiwa katika ujenzi.

"Kwa awamu ya tatu ya kutoka Kariakoo hadi Gongo la Mboto, mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ameshapatikana tangu Machi, mwaka huu,"alisema.

# Walimu wahoji michango CWT miezi 42

**Na Faustine Feliciane**

BAADHI ya walimu ambao ni wanachama wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), wamehoji matumizi ya michango yao kipindi cha miezi 42 tangu alipoingia madarakani aliyekuwa katibu mkuu wa chama hicho, Deus Seif.

Kutokana na hoja hiyo, CWT imewataka walimu hao kusubiri mkutano mkuu utakaofafanua kila kitu.

Mmoja wa wanachama wa CWT, ambaye hakutaka jina lake kutajwa gazetini, alisema mwaka jana viongozi waandamizi wa chama hicho, Deus na Mweka Hazina wa Taifa, Abubakari Alawi, walikamatwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na kushtakiwa kwa madai ya uhujumu uchumi na matumizi mabaya ya ofisi.

Alisema, kwenye kesi hiyo ya jinai namba 39/2021 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, moja ya tuhuma zilizowakabili ni kutumia fedha za chama zaidi ya Sh. milioni 13 kama gharama za usafiri, malazi na posho za kujikimu kwenda kuangalia mechi ya soka kati ya timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) na Cape Verde nchini Cape Verde.

"Lakini ukiangalia katika kipindi cha miezi 42 ambayo mtendaji mkuu alikuwa madarakani na mweka hazina, walimu tumechangia zaidi ya Sh. bilioni 30 ambazo zilitokana na kukatwa asilimia mbili kwenye mshahara wa kila mwalimu. Hatujui hizi fedha kama zipo au la hasa tunapoona viongozi ambao walihukumiwa kifungo cha miezi sita wakitumikia kifungo cha nje," alisema.

Pia alisema mahakama katika hukumu yao Juni 28, mwaka huu, (nakala ya hukumu Nipashe inayo), iliagiza washtakiwa mbali na kutumikia kifungo pia walitakiwa kurejesha fedha hizo ambazo ni mali ya CWT.

"Sasa wako nje inasemekana wanatumikia kifungo cha nje. Binafsi sina utaalamu wa sheria lakini hii haijakaa sawa. Vipi fedha walizotakiwa kurejesha? Pia katika michango ambayo tunachanga kila mwezi asilimia 30 inaingia kwenye uwekezaji wa chama, lakini tangu kuingia madarakani aliyekuwa katibu mkuu wetu (Seif) ambaye alikaa kwa miezi 42 hakuna uwekezaji wa wazi ulioonekana. Je, fedha za michango yetu zipo?" Alisema.

Mwalimu mwingine kutoka mkoani Tanga (jina linahifadhiwa), alisema katika kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi), CWT iliazimia kuchukua mkopo wa Sh. bilioni 4.6 za kununua fulana na gharama zingine kuelekea hafla hiyo.

"Lakini baadaye wakatuambia kwa kuwa chama kinajipanga kujenga makao makuu jijini Dodomaa. Fulana zitanunuliwa kwa walimu walioko jijini Dodoma pekee lakini baada ya hapo hatujaona uwekezaji huo wa ujenzi wa makao makuu. Haya yote tunahitaji ufafanuzi kwa sababu ni michango yetu inayotumika," alisema.

Naye mwalimu kutoka Kigoma alisema kila mwanachama wa CWT anakatwa asilimia mbili ya mshahara wake kama ada ya uanachama na walimu wasio wanachama wanakatwa asilimia mbili ya mishahara yao kama ada ya uwakala kwa mujibu wa Sheria Na 6 ya Kazi na Uhusiano Kazini ya mwaka 2004 na kila kila mwezi chama kinapokea michango hiyo.

Kutokana na makato hayo, alisema chama kinapata zaidi ya Sh. bilioni 4.5 kila mwezi na kwa utaratibu wa CWT, asilimia 30 ya mapato ya kila mwezi ni kwa ajili ya uwekezaji unaohusisha ujenzi wa majengo mapya na ukarabati wa majengo ya chama yaliyopo sasa.

"Walimu tunataka kujua tangu Mwalimu Deus kuingia madarakani na kumkuta mweka hazina wake mwaka 2019 mpaka 2022 ni miezi 42. Kwa hesabu ya kawaida zinakusanywa Sh. milioni 720 kila mwezi na ukiangalia kwa miezi 42 ni zaidi ya Sh. bilioni 30. Walimu wanataka kujua ziko wapi?" Alihoji.

Kutokana na madai hayo, Kaimu Rais wa CWT, Mwalimu Dinah Mathamani, aliwataka walimu kusubiri mkutano mkuu utakaofafanua malalamiko yote.

Alisema michango yote ya CWT inatumika kwa utaratibu wa katiba ya chama na maelezo yanatolewa kwenye mikutano ya chama kuanzia ngazi ya wilaya mpaka taifa.

Alisema kuelekea mikutano hiyo, tayari wameingiza Sh. bilioni 2.5 awamu ya kwanza kwenda kwenye wilaya kwa ajili ya mikutano hiyo lakini awamu ya pili wataziingizia wilaya Sh. bilioni 1.2 kufanikisha mikutano hiyo.

"Kuhusiana na ujenzi wa makao makuu ya chama ni kweli mpango huo upo. Awali baraza kuu la chama lilipitisha kuchukuliwa mkopo wa Sh. bilioni tano na kati ya hizo, Sh. bilioni mbili zilipangwa kutumika kwenye hatua ya awali ya ujenzi wa makao makuu ya chama Dodoma," alisema.

"Bahati mbaya mkopo huo haukuchukuliwa kwani taratibu hazikuwa zimekamilika kwa sababu aliyekuwa akifuatilia ni mtendaji mkuu wa chama ambaye ni Katibu Mkuu. Kama tunavyofahamu Katibu Mkuu (Mwalimu Deus) alipata matatizo na kufungwa, hivyo, mchakato ule ukawa umesimamia pale. Hiyo ndiyo sababu ya kuchelewa kuanza mradi ule wa ujenzi wa makao makuu ya chama Dodoma," alibainisha.



Ofisa Mwandamizi wa Uhusiano wa Jamii GGML, Shunashu Musa (kulia), akimkabidhi magodoro 50 msimamizi wa kituo cha wazee Bukumbi, Jonas Tarimo. Anayeshuhudia ni Ofisa wa GGML, Fredrick Musa (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wenye ugumba wapata mtetezi dhidi ya ukatili

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wagumba Tanzania (CCWTZ), kimesema kitahakikisha kinasimamia haki za wagumba ili waweze kuondokana na ukatili kutoka kwenye jamii na familia.

Mwenyekiti wa chama hicho, Shamila Makwenjula, akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu kuanzishwa kwa chama hicho na kasi ya kuielimisha jamii, alisema kwa ujumla kundi hilo limesahaulika na kupitia chama hicho watahakikisha kinasaidia wanawake na wanaume wagumba kutoa elimu kwa jamii ili waondokane na manyanyaso.

Makwenjula, alisema baadhi yao wanakutana na vipigo na msongo wa mawazo.

"Wapo wagumba wanaotengwa na familia zao na kuwasababishia kuathirika kisaikolojia na hii ni kwa wanawake na wanaume, kuna ambao hufikia hatua ya kukata tamaa ya kuendelea kuishi.

"Wengine hukatisha maisha yao na baadhi hufikia hatua ya kuiba watoto kwa lengo la kurejesha amani ndani ya familia zao."

Makwenjula alisema, CCWTZ pamoja na mambo mengine inatoa elimu kwa kushirikiana na wataalamu wa saikolojia na madaktari ili kuhakikisha jamii inakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kundi hilo.

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Kassim Pazi, alisema ndani ya mwaka huu wanatarajia kukizindua rasmi chama hicho ili kuendeleza utoaji wa elimu na kuiomba serikali ya Tanzania Bara na Zanzibar kuwaunga mkono.

# M/kiti TAMWA ataja mikakati kuinua wanahabari wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jitihada za kuwainua wanahabari wanawake na kuwahamasisha kuipenda taaluma yao, Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), kimetangaza mikakati ya kuwarudisha tena kwenye taaluma wanawake waandishi 'waliokwazika'.

Akizungumza na Nipashe muda mfupi baada ya kuchaguliwa tena kukiongoza chama hicho, kwa kipindi kingine cha miaka mitatu, Mwenyekiti Joyce Shebe, alisema katika miaka ya hivi karibuni tasnia ya habari imepitia misukosuko iliyoathiri waandishi, lakini wanawake zaidi.

Alisema, hali hiyo imesababisha wengi kuondoka kwenye 'media' na kwamba chama kimelenga kutumia mbinu mbalimbali kuwafikia na kuwarejesha kwenye taaluma yao.

Alisema kuwa utafiti uliofanyika karibuni ulibaini kuwa matatizo ya COVID-19, kubinywa uhuru wa vyombo vya habari na changamoto ndani ya 'media' kulisababisha tasnia kuyumba, kufunga uzalishaji na kupunguza wafanyakazi.

Hatua hiyo imeathiri zaidi wanawake walioondoka kazini na sasa idadi yao imepungua mno jambo ambalo TAMWA na wadau wengine wana wajibu wa kuwasaidia wanataaluma hao kurejea na kufurahia kazi zao.

"Wanawake wengi wamepungua kwenye 'media' tunaazimia kuwarudisha na kuwashauri waliopo wasiache na wajizatiti na kazi. Tatizo la uhuru wa kujieleza lilizidi. Vyombo vya habari kuminywa, kufungiwa na kukwama matokeo yake yamekuwa mabaya kwa wanawake kuachishwa au kuacha kazi," anakumbusha Joyce.

Alisema kuwa, TAMWA itafanya juhudi kuwasiliana nao ikibidi kukutana nao pia kuwafikia wanahabari wanawake vyuoni kuwahimiza wasikate tamaa.

"Kama itawezekana pia tutazungumza na wamiliki wa 'media' ili kuwaomba kuwe na mazingira sawa ya wanawake na wanaume kuwe na sehemu za kazi 'zinazofeva' jinsia zote mbili ili wanawake wasiachwe nyuma," alisema.

Aliwahamasisha wanawake waone kuwa kazi hiyo ni ya wote na uandishi uonekana kuwa sehemu sahihi ya kufanya kazi na kumudu maisha yao.

Kadhalika, ameahidi kuwa TAMWA itaendelea kuwa karibu na wanachama wake na kuangalia wanachopungukiwa na wanachohitaji kwa upande wa teknolojia na taaluma.

"Uandishi wetu unahitaji teknolojia na ubobezi au kujikita kwenye eneo unaloandikia. Hilo halikwepeki. Tutawahamasisha kubobea kwenye habari ziwe za siasa, uchumi, mazingira, afya na tabianchi ili kuwa na wigo mpana, pia kutumia teknolojia za mawasiliano kuwafikia wateja wao."

Kikubwa ni watu kutumia teknolojia ya habari kuchangamkia fursa zilizopo kwenye maeneo mbalimbali ili kunufaika na taaluma iwe ni kwa kujiajiri, kuajiriwa, biashara na kutoa huduma ili kufikisha taarifa zetu," alisisitiza.

# Viziwi walalamika makarani sensa kutojua lugha ya alama

Na Jenifer Gilla

WAKATI jana ikiwa siku ya mwisho ya sensa na kundi kubwa la Watanzania likifurahia kuhesabiwa, hali ni tofauti kwa makundi maalum ya wenye ulemavu.

Akizungumza, na Nipashe mmoja wa viziwi hao, Aneth Isaya, alisema ilikuwa akose kuhesabiwa baada ya karani aliyemtembelea kuahirisha kutokana na kushindwa kuwasiliana. Aneth ambaye pia ni Mkurugenzi wa Shirika la Furaha ya Wanawake Wajasiriamali kwa Viziwi Tanzania (FUWAVITA), alisema baada ya karani kuwasili nyumbani kwake alimsalimia kwa lugha ya alama ambayo ilimuwia vigumu kuielewa na kuishia kucheka.

Hali hiyo imeiwaibua baadhi watu katika kundi hilo wanaolalamikia changamoto wanazopitia kwa kukosa haki ya msingi kutokana na kutembelewa na makarani wasiojua lugha ya alama.

"Akatoa kishkwambi anachotumia kukusanya data akanionyesha kwa ishara kuwa utasoma hapa na utajibu maswali. Nilifanikiwa kujibu maswali ya mwanzo tu nikashindwa kwa sababu yalikuwa mengi na mengine yanataka ufafanuzi, akanionyesha picha ya mume wangu ukutani na kuniuliza yupo wapi?" Aneth alisimulia.

Aliongeza kuwa karani huyo alimpigia simu mume wake na kumueleza kuwa atakuja siku inayofuata kwa sababu wameshindwa kuelewana, kitendo kilichomshangaza kuwa kama asingekuwa na mume au msaidizi yeyote nyumbani asingepata huduma hiyo.

"Kitendo cha karani kuondoka kilinipa maswali mengi na kunifanya niwawazie wenzangu ambao hawaishi na wenza au ndugu majumbani mwao, nikajiuliza je, ni viziwi wangapi watashuhudia makarani wakiwapita kwa sababu ya changamoto ya mawasiliano?" Alihoji Aneth.

Naye, Salma Omari, alisema alilazimika kuongea na karani akiwa mbali ili kumsaidia mama yake ambaye ni kiziwi kuhesabiwa kutokana na changamoto ya mawasiliano kwa kuwa karani aliyemtembelea hakuwa na utaalam wa kuwasiliana naye hali iliyosababisha shughuli hiyo kuchukua muda mrefu kukamilika.

"Ilinibidi nisimamishe shughuli za ofisi kwanza nimsadie mama aliyepo mkoani ili apate huduma kwa sababu walikuwa hawaelewani kabisa na karani. Karani alikuwa analalamika kwa nini mmemuacha mama yenu peke yake wakati mnajua hasikii, nikamjibu kutokusikia sio ulemavu wa kusema ukae na mtu saa 24," alisema.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Ernest Kimya, alisema waliweka utaratibu mzuri kwa kuandaa na kuwezesha wataalam wa kuhudumia kundi hilo ili kuhakikisha kila mwenye ulemavu anahesabiwa.

Vile vile, alisema walitoa taarifa kuwa kama kuna mwenye ulemavu atapitia changamoto itakayosababisha asihesabiwe aiwasilishe kwenye kundi la whatsap na mpaka shughuli hiyo inaelekea ukingoni jana, hawajapokea malalamiko yoyote kutoka kwa kundi hilo.

"Tuna group (kundi) la taarifa la walemavu, kama kuna changamoto yoyote kama ni kiingereza au lugha ya alama, na tunatatatua changamoto hizo kwa haraka sana. Kwa hiyo kama kuna yeyote ajue kuwa hajachelewa kwa kuwa leo ndio siku ya mwisho, aseme yupo wapi ili tumtume karani aende kumhesabu," alisema.



Mkazi wa Kipunguni jijini Dar es Salaam, Bhoke Mussa, akihudumia moja ya bustani zake za mboga juzi. Bhoke ni ngariba mstaafu aliyepewa matuta 24 ya bustani na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, ili ajishughulishe na kilimo cha mboga mbalimbali ajiingizie kipato baada ya kuacha kazi hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wapigwa marufuku kuchinja, kula 'kitimoto'

Na Elizabeth John, NJOMBE

WANANCHI wa Kata ya Tandala, wilayani Makete Mkoani Njombe, wamepigwa marufuku kuchinja nguruwe na kula nyama kwa muda usiojulikana kutokana na uwapo wa ugonjwa wa homa ya nguruwe.

Ofisa Mifugo na Uvuvi, wilayani humo, Aldo Mwapinga, alitoa amri hiyo kutokana na vifo vya nguruwe 21.

"Kata ya Tandala kumeripotiwa dalili za ugonjwa wa homa ya nguruwe kwa hiyo tunaendelea na jitihada za kuhakikisha tunashirikiana na watendaji kuanzia ngazi ya kata hadi vitongoji kutoa taarifa juu ya hali inavyoendelea," alisema.

Alisema: "Baada ya kupata taarifa hizi tumesimamisha zoezi la uchinjaji wa nguruwe katika kila eneo la kata ya Tandala, na pili kutoa nguruwe kuwapeleka kwenye maeneo mengine, pia tumezuia utoaji nguruwe kutoa zizi moja kwenda jengine kwa ajili ya kupandisha kwa jike," alisema Mwapinga.

Mwapinga, aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano pamoja na kutekeleza maagizo yote yanayotolewa na wataalamu wa mifugo ikiwamo kuacha kufukua nguruwe waliofukiwa baada ya kufa, kuwachinja na kwenda kuuza nyama hizo vilabuni nyakati za usiku.

"Nawaomba wananchi watupe ushirikiano kwa kutupa taarifa kila kifo kinachotokea, kuacha kufukua mizoga ili kuhakikisha jamii yetu inakua salama kwa kufuata maelekezo," alisema Mwapinga.

Alisema, inawezekana kuutokomeza ugonjwa wa homa ya nguruwe na kuwa historia katika maeneo yao.

## Wananchi Likong'o kunufaika fursa mradi gesi asilia

**Na Said Hamdani,** LINDI

JAMII mkoani Lindi imetakiwa kuchangamkia fursa za kiuchumi ukiwamo ujenzi wa mradi wa kuchakata gesi asilia (LNG), unaotarajia kujengwa eneo la Likong'o.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Balozi Ombeni Sefue, ametoa rai hiyo, alipozungumza na viongozi wa wilaya na Mkoa wa Lindi, wakati wa ziara yake kuona eneo lililotengwa kwa ajili ya kujengwa kiwanda hicho.

Alisema, mradi wa kuchakata gesi asilia utakapoanza kujengwa, idadi kubwa ya watu watafika kufuata ajira na kwamba ni muhimu wananchi wakafahamu fursa zinazotarajia kufika kwao pamoja na kujiandaa kuzichangamkia.

Balozi huyo alisema, mradi huo utakapochanganya utanufaisha watu wa Manispaa ya Lindi na vitongoji vyake ikiwa ni pamoja na kuubadilisha mandhari kwa wananchi kushiriki shughuli mbalimbali za kiuchumi zitakazokuwa zinaendelea.

"Wito wangu wananchi wajiandae kufahamu fursa zinazokuja mbele yao, kwani haitoshi kuwapo kwa mradi tu, lazima watu wajiandae sasa," alisema Balozi Sefue.

Mwenyekiti huyo wa Bodi ya TPDC, alisema ni vizuri wananchi wakaendelea kuzalisha bidhaa zenye viwango vinavyohitajika kwa jamii na kuona faida ya kuwapo karibu na mradi mkubwa kama huo.

Alisema, moja ya kipaumbele cha Bodi ya TPDC na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ni pamoja na kuona utekelezaji wa mradi huo unaanza na wananchi wameusubiri kwa muda mrefu.

Vile vile, alifafanua kwa upande wa Bodi hiyo mpya, kipaumbele kikubwa ni kuwekeza nguvu eneo hilo la mradi wakati majadiliano na wawekezaji yanaenda vizuri hadi kufikia mwezi Desemba mwaka huu, yataweza kukamilishwa.

Alisema miaka ya nyuma walizoea kuona mwekezaji anapofika nchini kuwekeza vitega uchumi, miongoni mwa wajibu wake ni kujenga vyumba viwili vya madarasa na zahanati, lakini kwa sasa serikali imeenda mbali zaidi, ikiwamo kuona faida ya kiuchumi mradi ulipo.

Mwenyekiti huyo aliwasisitiza wazazi kusomesha watoto wao, masuala ya ufundi ili wanapomaliza wawe tayari kuajiliwa kwenye huo mradi uliopo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, alisema taratibu hizo zimeshaanza na zinaendelea kutekelezwa, baadhi wameshapata ujuzi kupitia Chuo cha Ufundi Stadi (VETA).

# Serikali yaandaa mwongozo matumizi endelevu ya mkaa

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii inaandaa mwongozo na mkakati wa taifa wa matumizi endelevu ya mazao ya mkaa ili kuhakikisha unapovunwa, hutumiwa hadi kufikia masoko uwe kwa njia endelevu.

Mwakilishi kutoka wizara hiyo Idara ya Misitu na Nyuki, James Nchare, alisema hayo jana wakati akifunga warsha ya siku mbili ya wadau wa misitu iliyoandaliwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uswizi (SDC) wakijadili masuala ya kuthibitisha mazao ya mkaa.

Nchare alisema suala la uthibitishaji wa mazao ya misitu ni moja ya ajenda zilizopo kwenye mkakati wa sera ya taifa ya misitu ya mwaka 2021-31 ulioainisha umuhimu wa kuthibitisha mazao ya misitu na mkaa ambao umeweka malengo maalum ya kufikiwa ifikapo mwaka 2031.

Alisema kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo Shirika na Mfuko wa Wanyamapori duniani (WWF) na TFCG wana lengo la kuthibitisha mazao hayo ili kusaidia kuongeza thamani pamoja na ubora ili jamii na serikali zinufaike kutokana na mapato kama yakizalishwa kwa ubora.

"Ukiwa na mazao ya misitu yaliyo bora ni sehemu ya uhifadhi kwa sababu ukitumia mlango uliotokana na mazao bora ya misitu hutobadilisha kwa muda mfupi kama ungetumia mlango unaotokana na mazao ya misitu yasiyo bora na kwamba ufanisi, tija na ubora katika uzalishaji wa zao la misitu ni jambo la msingi sana," alisema Nchare.

Aidha, Nchare alisema licha ya serikali pamoja na juhudi zinazoendelea kupitia Wizara ya Nishati kuendelea kuhamasisha matumizi mbadala ya mkaa badala kutegemea misitu kutumia umeme au gesi, pia inaona uandaaji wa mwongozo huo ukifuata mnyororo wa thamani utasaidia kusimamia uvunaji endelevu na kuhifadhi misitu.

Alisema Watanzania zaidi ya asilimia 85-90 wanategemea nishati ya mkaa kwa matumizi na inamaanisha kuwa bado mkaa unatakiwa kutumiwa na kusisitiza matumizi hayo yawe kwa njia endelevu bila kuathiri mazingira na misitu.

Alisema kuna changamoto ya kutofautisha mkaa uliovunwa kihalali na usiovunwa kihalali katika eneo la masoko jambo ambalo ni tatizo katika udhibiti, lakini mbinu zilizoainishwa zikisimamiwa zitasaidia kutambua mkaa upi ni halali na usio halali.

Naye Ofisa Mwezeshaji kutoka TFCG, Simon Lugazo, alisema kuwapo kwa mipango ya kisera na kisheria katika masuala ya uthibitishaji wa mkaa yanayoandaliwa kutasaidia mazao ya mkaa kupata manufaa ikiwamo masoko bora ya ndani na nje ya nchi.

Alisema kwa Tanzania tayari uthibitishaji umeshafanyika kwa Shirika la Mpingo (MCDI) kwa upande wa mbao na na upande wa mkaa bado hakuna aliyethibitisha, wanaona ni vyema kuelimishana zaidi uthibitishaji ili watu waweze kuutambua.

Awali, akizungumza kwa njia ya mtandao kwenye warsha hiyo akiwa nchini Kenya, Mkurugenzi wa masuala ya uthibitishaji Afrika, Dk. Harrison Ojwang, aliwataka wazalishaji mkaa kutambua umuhimu wa kufanya uthibiti bila kujali gharama.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wakili Amon Mpanju (kushoto), akikagua eneo la kilimo cha mboga katika makazi ya wazee Misufini mkoani Tanga, wakati wa ziara ya manaibu makatibu wakuu kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Wizara ya Maji katika makazi hayo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madereva kuelimishwa madhara ya pombe na vyombo vya moto

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imezindua programu ya kutoa elimu ya madhara ya kutumia vileo (pombe) na kuendesha vyombo vya moto kwa njia ya mtandao inayojulikana 'Wrong Side of the Road'.

Akizungumzia elimu hiyo, Mkurugenzi wa Mahusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, alisema kampuni hiyo imekuwa ikiendesha kampeni mbalimbali zinazohusu matumizi ya pombe ikiwa ni pamoja kutoa elimu ya unywaji kistaarabu.

Elimu hiyo itakayotolewa kupitia video ya ushuhuda wa mwathirika wa unywaji pombe na kuendesha chombo cha moto inalenga kubadilisha tabia za madereva ambao hutumia vilevi na kuendesha vyombo vya moto.

"Lengo la elimu hii tunayotoa ni kuwabadilisha madereva. Tunalenga kupunguza idadi ya madereva wanaokunywa na kuendesha vyombo vya moto na ambao wana mtizamo hasi kuwa kunywa na kuendesha ni jambo la kawaida. Video inaelezea kilichompata dereva anayetoa ushuhuda ikilenga kuwaonyesha hatari inayomkabili dereva anayekunywa na kuendesha," alisema.

Pamoja na kutoa elimu kwa umma kwa njia ya mtandao, video hiyo inaelezea madhara yanayotokana na uamuzi usio wa busara wa kunywa na kuendesha huku ikisisitiza kuwa si salama kunywa na kuendesha.

"Tunayo furaha kuzindua njia hii ya aina yake ya kufikisha ujumbe kwa maelfu ya Watanzania popote pale walipo. Kutumia kilevi na kuendesha chombo cha moto sio tu ni jambo la hatari kwa dereva bali hata kwa watumiaji wengine wa barabara na tunapenda kuona watu wakibadilika juu ya hili," alisema.

# WAJIKI yaanzisha kampeni kukabili rushwa ya ngono

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), linatarajia kuendeleza kampeni yake ya kupinga rushwa yxa ngono kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mwezi ujao.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Janeth Mawinza, alisema kampeni hiyo inayoongozwa na kaulimbiu ya 'Safari salama bila rushwa ya ngono inawezekana', itafanyika katika wilaya tatu mkoani Dar es Salaam.

Alitaja wilaya hizo kuwa ni Kinondoni, Ilala na Temeke huku akifafanua kuwa shirika lake limepata ruzuku ya Sh. milioni 80 kwa ajili ya kuendeleza kampeni hiyo katika vipindi viwili vya mwaka 2022/2023.

"Tumepata ruzuku ya kuendelea kampeni yetu kutoka Women Fund Tanzania Trust (WFT-T), hivyo mwezi ujao tutaendeleza kampeni ya 'Vunja ukimya safiri salama bila rushwa ya ngono kwa wasichana na wanafunzi inawezekana' itaanza," alisema Mawinza.

Mawinza alisema mradi huo umeshapokewa na kupewa baraka zote na TAMISEMI wakati wa uwasilisho wake na kutambulishwa na kupata kibali cha serikali, jijini Dodoma hivi karibuni.

Kampeni hiyo itahusisha utoaji wa elimu ya jinsi ya kuepuka vishawishi vya rushwa hiyo na kutambua viashiria vyake, semina, mikutano na pia kutembelea vijiwe vya madereva wa bodaboda, bajaj na daladala.

"Kwa kawaida kampeni hiyo huwa tunashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo TAKUKURU, madereva wa bodaboda, bajaj, daladala na maofisa wa ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii," alisema.

Mawiza alifafanua kuwa madereva wa vyombo hivyo vya moto ndiyo wanaotuhumiwa kuhusika, katika rushwa hiyo kwa kutumia lifti kuwanasa kirahisi wanafunzi na wanawake.

Alisema shirika lake tayari lina baadhi ya madereva hao ambao sasa ni mabalozi wa WAJIKI na wanahamasisha vita dhidi ya rushwa ya ngono katika maeneo mbalimbali ya wilaya hizo tatu.

"Kwa mfano kuna Umoja wa Madereva wa Wilaya ya Kinondoni (UWAMAWIKI), Umoja wa Madereva wa Daladala Makumbusho, Tegeta na Bunju (UWAMATEBU,) Umoja wa Madereva wa Daladala Makumbusho- Posta (UWAMAPO,) Umoja wa Madereva wa Daladala Mbagala (UMDM,) na Umoja wa Madereva na Pikipiki na Bajaji Gongolamboto," alisema.

Alisema hata madereva wa bajaji wana umoja pia na wanatoa elimu ya kupiga vita rushwa ya ngono katika vijiwe vyao.

Nipashe
TESA
Jumanne Agosti 30, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Fahamu namna ya kupunguza kero, migogoro kwenye familia



Ukurasa 13



Ukurasa 12

Kasi ya wanafunzi kunaswa mtego mimba utotoni inatisha

SAYANSI

**NA MWANDISHI WETU**

# Moto wa nyika ulivyo maangamizi kwa wanyama, mimea na kitisho cha utalii



Swala 'oryx' na miti ya 'erica arborea' bayoanuai inayopatikana Mlima Kilimanjaro pekee. :**PICHA ZOTE:MTANDAO**

MOTO wa nyika ni moto unaowaka bila kupangwa na wakati mwingine usiodhibitiwa wala usiochagua pakuwakia, unaweza kulipuka popote iwe mijini au vijijini.

Hivi karibuni mataifa ya Ulaya yakiwa kwenye kiangazi kilichoambatana na joto kali linalozidi nyuzi 42 kwa mfano nchini Uingereza zilipata pia changamoto ya moto wa nyika.

Nchi za Romania, Austria, Ujerumani, Ureno na Afrika Kaskazini na mataifa ya Algeria na Tunisia ni miongoni mwa maeneo yaliyotishiwa na moto wa nyika uliosababishwa na joto hilo kwenye ukanda wa Mediterranean.

Moto wa nyika ni habari zinazosikika kwa kasi hasa miezi ya hivi karibuni.

Inaripotiwa kuwaka Ulaya na Marekani pamoja na Afrika Kaskazini, lakini ukiambatana na mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo si jambo geni sana kwa Tanzania kwani limewahi kutokea katika Mlima Kilimanjaro na kusababisha uharibifu wa bayo anuai.

Moto huo unaibua maswali mengi kama chanzo chake ni nini? Au ni muujiza? Inawezekanaje moto kuwaka bila kuwashwa?

Hakuna majibu ya moja kwa moja kwa sababu kawaida moto husababishwa na shughuli za binadamu kama kuvuta sigara, kuchoma nyasi kusafisha mashamba au hitilafu ya umeme lakini kwenye jambo la asili (natural phenomena) kama vile radi inapochoma miti, makazi na viumbe.

Kwa mujibu wa mtandao wa EarthOrg, asilimia 50 ya moto wa nyikani unaoripotiwa kuwaka sehemu mbalimbali chanzo chake hakifahamiki wala jinsi au namna ulivyoanza.

Ila, kutokana na mabadiliko ya tabianchi moto wa nyikani wakati huu unachochewa na ukavu na ukame mwingi maporini unaoambatana na upepo mkali.

Moto wa nyikani umetokea Oktoba mwaka 2020, kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro, ukianzia kwenye eneo lenye nyasi kavu na kusambazwa kwa kasi sehemu nyingine kutokana na upepo mkali uliokuwa unavuma.

Moto una athari kwa Kilimanjaro kwa sababu mlima ni nyumbani au makazi ya kipekee ya mimea, wanyama na wadudu kwa hiyo moto huo unapotokea inamaanisha una athari kubwa kwa bayoanuai na kuharibu mfumo wa kiikolojia.

Aidha, mlima huo unaotokana na 'volcano iliyotulia' una mimea na wanyama, wasiopatikana popote duniani, hivyo moto wa asili unapotokea unaangamiza rasilimali hizo.

Kwenye milima huo mrefu zaidi barani Afrika ambao upo kwenye mazingira ya kitropiki, kadiri unavyopanda juu zaidi, ndivyo unavyokuwa na 'spishi nyingi zaidi,' za mimea, wadudu na wanyama.

Ni mimea na wanyama gani wanaoishi mlimani humo pengine ni swali mtu analoweza kujiuliza. Aina kubwa zaidi ni miti ya 'erica arborea' na 'oryx' jamii ya swala, ambavyo ni vitu maalumu vya mlima.

Miongo kadhaa iliyopita, miti ya erica yenye urefu wa hadi mita 15 ilipatikana Kilimanjaro, lakini sasa mvua imepungua na moto wa mara kwa mara, vimebakia vichaka vyenye urefu wa mita mbili na ukanda wa msitu unapungua, ikiwa ni athari ya moto wa nyika.

Utafiti wa karibuni unaonyesha kuwa ukungu kwenye mlima unaweza kuwa ufunguo wa maisha ya miti hiyo, hasa wakati wa kiangazi, ambao unatanda kuanzia Mei hadi Oktoba. Ukiwa kwenye mwinuko wa juu hufidia unyevunyevu kwenye majani ya mimea, ambayo hudondoka chini kwenye udongo na kuongeza furaha ya mimea.

Moto wa nyika unakwamisha ukungu kutokea. Hii inasababisha kupungua kwa maji chini ya ardhi, ambayo ni muhimu kwa mimea na wanyama kwenye tambarare zinazozunguka mlima.

Na moto huharibu miti, ingawa mchakato wa miti na misitu kuchipuka wakati wa msimu wa machipukizi ni wa kawaida unaoruhusu mimea kukua tena kila mwaka. Lakini kiwango cha moto wa porini kikiwa kikubwa sana kinaongeza wasiwasi wa kuchipuka.

ELIMU

NA CHRISTINA HAULE, MOROGORO

# Kasi ya wanafunzi kunaswa mtego mimba utotoni inatisha

## Walezi, wazazi wapashwa 'mnajisahau'



Wanafunzi wa kike na wa kiume wanagharamiwa elimu na serikali, familia ziwasaidie wasibaki nyuma. **PICHA :CHRISTINA HAULE**

OFISA Ustawi wa Jamii Mkoa wa Morogoro, Jessica Kagunila, anapowatazama wazazi na walezi, anaona wamesahau wajibu wao wa kuwalea na kulinda watoto, ndiyo maana ukatili wa kijinsia zikiwamo mimba na ndoa za utotoni zinaongezeka kila wakati.

Anasema, mimba hizo zinaongezeka nchini akitupia jicho Morogoro kuwa kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2020/21 zimeongezeka mimba 433, na kukwamisha wasichana kielimu licha ya serikali kuigharamia.

"Mwaka 2019/2020, matukio ya mimba yalifikia 844. Ulanga mimba 518, Mlimba ni ya pili mabinti 75, Ifakara wako 73, Gairo ni 61, Manispaa 51, Mvomero 32, Morogoro 15, Kilosa 14 na Malinyi watano."

Anaeleza kuwa, mwaka 2020/2021 ziliripotiwa mimba 1,277, Ulanga zilikuwa 901, Gairo 211, Manispaa 79, Mvomero39, Morogoro 27, Ifakara 18 na Malinyi mbili.

Umri wa mabinti hao kwa mujibu wa Jessica, ni kati ya miaka 13 hadi 18 na katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu taarifa za watoto wajawazito 2,422 ziliripotiwa kwenye jamii, vituo vya afya na polisi.

Watoto hao wanatoka Wilaya za Mlimba 1,157, Ulanga 262 na Gairo 38, Morogoro Vijijini 14, Ifakara saba , Mvomero tisa na Manispaa ya Morogoro nane, yote hayo yakionyesha kuwa wazazi na walezi suala la elimu ya makuzi na maendeleo ya mtoto ni geni au si kipaumbele.

"Tubadilike tuache kusema tunajua kuzaa, kulea tunamuachia Mungu. Hapana si sahihi" anaonya na kutaka wazazi kutambua wajibu wao kwa watoto hasa malezi, kuwaepushia vishawishi vinavyowaingiza kwenye ukatili wa kijinsia kama mimba na ndoa utotoni.

Jessica anasema malezi duni, kuporomoka maadili na maingiliano na tamaduni mbaya za jamii zisizojali hatma na maendeleo ya watoto ni chanzo cha mimba hizo.

"Kwa mfano ngoma za vigodoro baadhi ya wazazi hawajaona kuwa hazina umuhimu wala hazimjengi mtoto wa kike katika maadili mema wanazidi kuzikumbatia." Anaongeza.

Anataka elimu ya kuepusha mimba za utotoni na kuhamasisha malezi bora kutolewa na wazazi, walezi, viongozi wa dini, wa serikali, kamati za ulinzi na usalama na zile za ulinzi mwanamke na mtoto wa kike zilizopo vijiji.

Mwanaidi Lwena, wa Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi mkoa wa Morogoro, anasema mimba na ndoa za utotoni zinahitaji kuwekewa mikakati madhubuti kwenye kutoa elimu.

Anasema, jeshi hilo linahamasisha jamii mitaani na wanajiandaa kuunda klabu za jenda na masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia katika sekondari 10 za kata za Manispaa ya Morogoro.

Klabu hizo zitawezesha polisi kutoa elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia na maana ya jenda, hatua hiyo itafanya wepesi wa kupata taarifa zozote za ukatili wa kijinsia dhidi ya wanafunzi ikiwa ni kutoka kwa walimu ambao wanadaiwa kuhusika na unyanyasaji kwa wanafunzi ambao hawana pa kusemea akiongeza kuwa Tanzania wasichana wanne kati ya 10 wanaoolewa chini ya miaka18.

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia idadi ya watu Duniani (UNFPA), asilimia 35, ya wanawake nchini wenye miaka 20 hadi 24 waliolewa kwa mara ya kwanza au walikuwa katika mahusiano kabla ya kutimiza miaka 18.

Kati ya mwaka 2000 hadi 2011, taasisi ya kimataifa ya 'Human Rights Watch', imeripoti kesi za wasichana wenye umri wa miaka saba kuozwa.

Asha Faraji (19), anayeishi Chamwino Morogoro, aliyepata mimba katika umri mdogo analalamika kuwa hali hiyo imezima ndoto zake na tangia mwanzo alitamani kupata elimu na kuwa daktari.

Akiwa kidato cha kwanza Sekondari ya Mgulasi huko Chamwino, alishawishika kutamani vitu kama chipsi na kuishia kupata mimba asiyoitarajia na kuacha shule.

Anasema, walianza maisha na mzazi mwenzake ambaye alikuwa fundi pikipiki na kwamba uhusiano ulivunjika mtoto alipofikisha miezi tisa kwa madai ya kukosa uaminifu.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigela, kabla ya kuhamishiwa Geita, akizungumzia ufumbuzi wa suala la mimba za utotoni, anasema moja ya mikakati ya serikali kukabili kuhakikisha watoto wenye umri wa kwenda shule wanapata elimu bila vikwazo.

Anasema 'kumkosesha elimu mtoto wa kike ni kumnyima haki yake ya msingi' akiwaonya wazazi na walezi kuacha mara moja kuwaoza.

Mkurugenzi wa asasi ya kiraia ya Wezesha Mabadiliko (WEMA) Dk. Lusako Mwakiluma, anawataka wanafunzi kuzingatia mbinu 10 za mafanikio ya maisha kwa muda mfupi na mrefu na kuachana na mambo yaliyo kinyume na maadili.

Mbinu 10 ni kuandika malengo ya maisha, nidhamu na utayari wa kufanya walichopanga kukitekeleza,kujali afya, muda, kuwa na taarifa sahihi zao na wengine, kuwa na marafiki sahihi, kusimamia mwelekeo wako,kujithamini, kujiamini na kujikubali.

Anasema WEMA, inatoa elimu kwa wasichana wakiwamo wanafunzi ili wajitambue na kuepuka mimba za utotoni kuanzia shule za msingi kwa imani kuwa msichana akijitambua hawezi kwenda kinyume na lengo lake na akihama kwenye lengo lake anahamia kwa la mtu mwingine.

Akizungumzia sheria ya ndoa ya mwaka 1971, anawakumbusha wabunge kuirekebisha ili iendane na wakati.

Shekhe wa Msikiti Mkuu wa Morogoro Twaha Kilango, akizungumzia kuhusu sheria ya ndoa anasema ni vyema jamii kutambua kuwa inafaa kumuozesha binti akiwa na uwezo wa kujimudu kwenye maisha ya ndoa.

"Mtoto apatiwe haki zake za msingi na kuolewa katika kipindi ambacho jamii haitalaumu kilichotokea na kwamba kumuozesha mtoto au kubebea mimba chini ya miaka 18 kwa karne ya sasa si jambo jema kwa vile uzazi katika umri mdogo ni hatari lakini pia anaweza kushindwa kuwahudumia watoto tatizo linapotokea."

Mwanafunzi wa kidato cha tatu Sekondari ya Uwanja wa Taifa, (jina tunalo), anasema wauza chipsi na bodaboda ni kundi hatari linaloongoza kuwapa mimba wanafunzi kwa kuwalaghai kwa vyakula bure na usafiri.

Taarifa za mtandao wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (UNICEF,) inasema kuna mafanikio makubwa ya kupungua ndoa za utotoni duniani ambapo inakadiriwa kuwa ndoa hizo milioni 25 zilizuiliwa miaka iliyopita.

Inasema, kwa sasa ni msichana mmoja kati ya watano anayeolewa chini ya miaka 18 tofauti na ilivyokuwa miaka iliyopita msichana mmoja anaolewa kati ya wane, na kwamba nchi za kusini za Bara la Asia zimepunguza ndoa hizo.

UNICEF, inasema kati ya 2010 na 2017, Tanzania ilikuwa ya tatu kwa kuwa na viwango vya juu vya ndoa za utotoni baada ya Sudan Kusini na Uganda na kwamba kwa Sudan Kusini kiwango cha watoto wa chini ya miaka 18 wanaoozwa ni asilimia 52 na nchini Uganda ni asilimia 40 na Tanzania ni asilimia 31.

Mikoa inayoongoza kwa ndoa hizo ni Katavi asilimia 45, Tabora 43 na Mara ni asilimia 37.

ELIMU

NA PANRAS LUOGA, MUHAS

# Fahamu namna ya kupunguza kero, migogoro kwenye familia



Kugombana wanandoa kunasababishwa wakati mwingine na usiri au kukosa ushirikishwaji kwenye masuala ya kifamilia. **PICHA: MTANDAO**

"USIFANYE maamuzi ukiwa na hasira, maumivu au furaha ya kupitiliza". Ndivyo wenye hekima wanavyokushauri.

Ukiangalia zama hizi kumekuwapo na ongezeko la taarifa za kutokea na kuendelea kwa matukio ya migogoro ya familia na kati ya sababu kubwa inaweza kuwa ni kutokuwapo kwa ushirikishwaji wa kutosha wa mwanafamilia au wahusika katika kutengeneza mipango yao.

Mfano, kutengeneza mipango ya matumizi ya nyumbani imekuwa kazi ya baadhi ya watu na kuwaacha wengine wakishangaa na kuwa watekelezaji, mara nyingi baba au mama peke yake, au wote wawili peke yao hutengeneza mipango bila kuwashirikisha wengine hasa watoto na wategemezi ambao mara nyingi ndiyo watekelezaji na waathirika wakubwa wa mipango hiyo.

Imetokea baba au mama peke yake anaamua shule gani mtoto akasome bila kumshirikisha mwanafunzi ambaye ndiye mhusika mkuu katika utekelezaji wa mpango wa masomo yake. Muda mwingine, mume anaamua kuuza ng'ombe bila kumshirikisha mke au watoto. Mama naye anapanga na kujiunga na kuchukua mkopo kwenye kikundi cha Kikoba bila kumshirikisha au kumwambia mume, watoto kuhusu mpango na malengo ya kukopa.

Mtoto anakuwa na mpango wa kurithi mali za wazazi bila hata kuwashirikisha wamiliki wa mali hizo. Yote hayo huleta migogoro ya kifamilia na hii ni kutokana na kukosekana kwa mawazo na kuungwa mkono kutoka kwa wengine hivyo kuleta ukakasi kipindi cha utekelezaji wake.

Kwa mfano, kumekuwa na visa vya baadhi ya wanafamilia kumiliki na kuendesha biashara, kununua vitu kama kiwanja au kujenga nyumba kwa kificho bila kuwashirikisha wengine.

Udhaifu huu kwa baadhi ya wanafamilia umepelekea ugumu katika kutambua mipango ya shughuli, matumizi ya rasilimali zake, jinsi mafanikio au kushindwa kulivyotokea na uwepo wa mabadiliko katika mipango ya jamii hizo.

ATHARI KUTOKUSHIRIKISHWA

Madhara yakutowashirikisha wanafamilia katika mipango ni kuwapo kwa migogoro ya kifamilia, kwanza huanza kwa kutengeneza migogoro ya ndani ya nafsi ya mtu mmoja mmoja mfano, mtoto ambaye hakushirikishwa katika mipango ya shule gani angetamani akasome au masomo gani akasome.

Hilo, litamfanya awe na mgogoro binafsi ndani ya nafsi yake kuhusu kuutekeleza mpango huo wa elimu kwani anakuwa anatekeleza kitu ambacho hakushiriki katika kukipanga hivyo kukosa mchango wa mawazo yake.

Mke anayepigiwa simu na mme wake kuwa kuna mtu anakuja kuchukua kuku au ng'ombe hapo bila yeye kushirikishwa mapema katika mpango huo lazima awe na mgogoro ndani ya nafsi yake. Mume anayeongewa mlango na wageni wanaokuja kumdai mke wake marejesho ya mkopo au kumpa taarifa za mke wake kushindwa kulipa mkopo na hivyo anakuja kuchukua vyombo vya ndani bila yeye kushirikishwa mapema katika mpango huo lazima apate mgogoro wa ndani ya nafsi yake mwenyewe.

Zaidi ya haya yote ushirikishwaji duni au kutokuwapo kabisa kwa ushirikishwaji katika kutengeneza na kutekeleza mipango ya familia huleta migogoro kati ya mtu na mtu kwa maana mwanafamilia mmoja na mwingine. Mara baada ya kuwa na mgogoro wa nafsi kinachofuata ni mgogoro wa mtu na mtu. Katika familia mgogoro baina ya wazazi au wazazi na watoto au mtoto na mtoto mwingine toka familia moja.

"Tukumbuke sana kuwa tunashauriwa na wataalamu wa saikolojia kuwa tusifanye maamuzi tukiwa na hasira au furaha ya kupitiliza".

Lakini hali hii ya kuwepo kwa migogoro ya nafsi au baina ya wanafamilia huleta hasira na kupunguza uwezo wa akili kufanya kazi yake kwa usahihi. Na hivyo kupelekea wanafamilia kujihusisha na matukio yasiyotegemewa na wanajamii kama kujiua kwa kujinyonga au kunywa sumu, kuuana, kujeruhiana, kutalikiana na muda mwingine kukimbia na kuziacha familia zao.

Matukio haya yamekuwa yenye madhara zaidi kwa wanawake na watoto kwani ni waathirika wakubwa wa migogoro ya kifamilia. Pengine ni kwa sababu ya umuhimu wa majukumu na nafasi zao katika familia.

Mfano, hata kama baba kwa maana ya mume atauza chakula chote pale nyumbani bila kumshirikisha mama, muda wa chakula ukifika watoto watakwenda kwa mama yao kuomba chakula. Hii zaidi inatokana na utamaduni na mazoea ya jamii nyingi na pia umuhimu wa majukumu ya mama katika kuendesha familia yake. Ikumbuke kuwa kutokea kwa matukio kama haya huongeza ule mgogoro wa nafsi kwa mama na watoto kwani hawakushirikishwa kwenye mpango wa kuuza chakula na sasa wanapata maumivu yanayotokana na kilichofanyika.

Na kuanza kuwa na chuki na yule ambaye ametengeneza mpango huo na kuutekeleza bila wao kushiriki wala kutoa mawazo yao. Mtu akifikia hatua hiyo, ndipo kila mmoja huweza kuchukua maamuzi tofauti kadiri ya uwezo wa kuvumilia na kumudu maumivu hayo.

Mfano, kujinyonga kwa mwanafamilia au kuuawa mwanafamilia mwenzake. Cha zaidi chuki hii huzidi na kuendelea kutengenezwa kila mara ambapo mhusika atakosa kushirikishwa katika mpango wa ndani ya nyumba na kupata madhara zaidi hasa kama utekelezaji utamletea maumivu au mateso katika maisha yake.

Ushirikishwaji wa wanafamilia katika kutengeneza mipango yao inaweza kufanywa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuweka wazi mipango, vipimo, vya mapato na matumizi katika familia. Mfano; wanafamilia wanatakiwa kushiriki katika kuweka mpango wa mwaka na vipimo wa vitu vinavyotumika nyumbani kama vile chakula (mchele au unga na maharage) kinachowatosheleza.

Kushirikishwa katika mipango ya biashara au shughuli yoyote ambayo mmoja wa wanafamilia anafanya ili kujua malengo, namna inavyoendeshwa, changamoto na mafanikio yake. Mfano, mzazi anayetaka kuuza nyumba basi awashirikishe wote na kupata mawazo yao ili kuboresha wazo na kurahisisha utekelezaji wa mpango huo. Pia mtoto, anayependa kwenda shule awashirikishe mpango huo wanafamilia wengine juu wapi anapenda kwenda kusoma, masomo gani na malengo yake ya baadaye ikiwa ni pamoja na faida na changamoto anazozitegemea katika kutekeleza mpango husika.

Hii husaidia kwani wanafamilia wote watakuwa wameshiriki na kutoa mawazo yao na kukubaliana au kuukataa mpango huo wa familia au mwanafamilia. Zaidi ya hayo yote nikuwa ushirikishwaji katika kuandaa mipango ya familia husaidia katika utekelezaji wa mipango hiyo hivyo kuondoa malalamiko kwa baadhi ya wanafamilia kwa kutoshirikishwa katika kupanga mipango ya kifamilia.

FAIDA USHIRIKISHWAJI

Kuna faida nyingi zitokanazo na ushiriki wa wanafamilia katika kupanga mipango ya maendeleo na matumizi kwa sababu toka mwanzo wa kuandaa hadi mwisho wa utekelezaji wa mpango wote washiriki na watoe mawazo yao na kushawishika kukubaliana na mpango utakaotengenezwa na familia ni kazi waliyoifanya wenyewe.

Baadhi ya faida ni kuongeza umiliki wa mipango yao na kurahisisha utekelezaji wake, kupunguza malalamiko kwa baadhi ya wanafamilia hivyo kuepusha migogoro ya ndani ya nafsi na baina yao na zaidi husaidia katika kufanya maamuzi sahihi ya kutengeneza mipango bora ya nini kifanyike na kwa wakati gani kwa maana ya nini kipewe kipaumbele zaidi na kipi kisubiri kidogo, kuongeza au kusitisha utekelezaji wa mipango fulani katika familia kutokana na mawazo ya wanafamilia wote kuamua jambo hilo na pia ni kupelekea kuondoa migogoro inayoonekana sasa.

***Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Afya Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili.***

***MAONI:0757645746.***

ELIMU

NA JOSEPH MWENDAPOLE

# TEA yawapa raha vijana, maelfu wapata ujuzi kuna ufundi kidijitali, wenye ulemavu wamo

VIJANA takribani 33,000 huenda hawatalalamikia kukosa ajira ni kwa sababu wamefunguliwa milango ya kujiajiri, kuajiriwa na kuajiri wenzao baada ya kupata mafunzo ya kuendeleza elimu ya ujuzi na stadi za kazi, yanayotolewa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Aidha, TEA inalenga kufikia vijana 38,000 nchi nzima kabla ya kuisha mwaka huu, jukumu linalofanywa na Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF), anaeleza Mkurugenzi Mtendaji wa mamlaka hiyo, Bahati Geuzye.

Akizungumza na Nipashe, anaeleza kuwa vijana wengi wamepokea mafunzo mbalimbali yanawawezesha kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha biashara, kujiajiri na kuajiriwa kupitia programu hiyo.

Hadi kufikia Julai 2022, wanufaika 33,510, wanaume 17,257 asilimia 51.5 na wanawake 16,253 sawa na asilimia 48.5 wamepatiwa mafunzo katika awamu mbili, anaongeza, Bahati.

Mfuko wa SDF, ni sehemu ya programu ya kuendeleza elimu ya ujuzi na mafunzo ya stadi za kazi zenye kuleta tija katika ajira na mpango mkakati wa kitaifa wa kukuza na kuendeleza ujuzi, unosimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mkurugenzi wa TEA, anasema lengo la Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi ni kuwezesha vijana kupata ujuzi utakaowawezesha kuajiriwa, kuajiri au kujiajiri.

Kadhalika, SDF inalenga kufadhili mafunzo ya kuendeleza ujuzi katika sekta sita za kipaumbele cha kilimo na biashara, utalii na huduma za ukarimu, uchukuzi, ujenzi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na nishati na kwamba mfuko unalenga kunufaisha vijana 38,000 nchi nzima kufikia Desemba mwaka huu.




Bahati Geuzye.

Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa miradi ya mfuko wa SDF, mafunzo yaliyojikita katika sekta ya kilimo na kilimo biashara, Shilingi bilioni 3.1 zilitumika kuwezesha taasisi 15 kutoa mafunzo ya ujuzi.

Anasema, awamu ya pili ya utekelezaji ilianza mwaka wa fedha wa 2019/20 na 2020/21, ikitumia Shilingi bilioni 9.7 kufanikisha miradi 81.

Anasema vijana 33,510 wamepatiwa mafunzo katika awamu mbili na kwamba Shilingi milioni 385.8 zimetolewa kunufaisha vijana 1,018 katika programu ya utarajari kwenye sekta za TEHAMA, utalii na huduma za ukarimu, nishati, ujenzi na uchukuzi.

Pia, SDF, inafadhili mafunzo ya ujuzi kwa wanufaika 4,000 kutoka kaya maskini na makundi maalum na kwamba ifikapo Desemba 2022, lengo ni kuwezesha vijana wa kaya maskini kupata ujuzi na kujikwamua kiuchumi kwa mujibu wa Bahati.

Anasema wanufaika 1,627 wameshapata mafunzo katika awamu ya kwanza ya mpango huo na awamu ya pili ya ufadhili inatarajiwa mwezi huu.

Kwenye awamu hiyo SDF inalenga wanufaika hadi Desemba mwaka huu vijana 2,373 kati yao 600 kutoka Zanzibar watakuwa wamepokea mafunzo, anasema.

Aidha, anasema wengine 474 watakuwa wenye ulemavu na kwamba wanafunzi wengine 1,299 watatoka Bara.

Mkurugenzi Bahati, anasema mafunzo ya kuendeleza ujuzi yanatolewa na vyuo vya ufundi stadi (VETA), vya Maendeleo ya Wananchi (FDC), Vituo vya Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo (SIDO) na Vyuo vya Mafunzo ya Amali Zanzibar.

Anabainisha kwamba, mfuko wa kuendeleza ujuzi pia umeanza kutekeleza ufadhili wa mafunzo ya kiubunifu kwa njia ya mtandao (innovative training through e-learning) unaolenga kutoa mafunzo ya ujuzi kwa njia ya mtandao kwa walengwa 4,305 ifikapo Desemba 2022.

Shilingi bilioni 2.3 zinatumika kugharamia programu hiyo inayolenga kutoa fursa kwa vijana kidigitali na taasisi 15 za kutoa mafunzo ya ufundi na ufundi stadi zilizopata ruzuku ya SDF zitatekeleza jukumu hilo.

"Kwa niaba ya bodi ya wakurugenzi, menejimenti na watumishi wa TEA, napenda kuishukuru serikali ya awamu ya sita ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutenga fedha kutekeleza miradi ya maendeleo chini ya Mfuko wa Elimu na Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi," anasema.

Aidha, ainaishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na pamoja na viongozi wakuu wa wizara kwa usimamizi, miongozo, na ushauri unaowezesha kutekeleza jukumu hilo.

Anasema TEA, inatekeleza majukumu yake kupitia mpango mkakati wa miaka mitano kuanzia mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26.

Vile vile utekelezaji wa miradi ya elimu unazingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa unaolenga kuendeleza rasilimali watu na huduma za kijamii ikiwamo upatikanaji elimu na ujuzi kwa wananchi.

## WANENAVYO MALENGA

## WATAALAMU WA TEHAMA

HAWASEMWISEMWI sana, lakini twawatumia,
Tunakwamakwama sana, shida watutatulia,
Kuna muda chaumana, wao watutanzulia,
Watalamu wa TEHAMA, pongezi zifike kwenu.
Dunia siyo ya jana, vile tuliitumia,
Analogi ni ya jana, digital imeingia,
Bila TEHAMA kuona, njiani utaishia,
Watalamu wa TEHAMA, pongezi zifike kwenu.
Sasa ni mifumo sana, maishani twatumia,
Na kwa kazi nyingi sana, ndiyo yatutatulia,
Ikibuma shida sana, simu tunawapigia,
Watalamu wa TEHAMA, pongezi zifike kwenu.
Watalamu bomba sana, taaluma watumia,
Wanawajibika sana, kwa asilimia mia,
Kwa vile wajua sana, nafasi washikilia,
Watalamu wa TEHAMA, pongezi zifike kwenu.
Iwe asubuhi sana, shida ikikuingia,
Mchana jioni sana, piga wanasaidia,
Na hata usiku sana, hawawezi kuchunia,
Watalamu wa TEHAMA, pongezi zifike kwenu.

Mwaupiga mwingi sana, kazi mnatufanyia,
Twaoneka bora sana, kazi yenu yachangia,
Tunawapongeza sana, ni wajibu furahia,
Watalamu wa TEHAMA, pongezi zifike kwenu.
Leo wala siyo jana, ilivyokuwa dunia,
Tumefika mbali sana, kwenye teknolojia,
Mhimili bora sana, ambao twautumia,
Watalamu wa TEHAMA, pongezi zifike kwenu.
Tunafanya mengi sana, TEHAMA tukitumia,
Mambo yaenda twaona, sante teknolojia,
Maendeleo twaona, ndiyo inasaidia,
Watalamu wa TEHAMA, pongezi zifike kwenu.
Kwa huduma bora sana, inaturahisishia,
Tena kwa haraka sana, inavyotusambazia,
Kule kucheleweshana, kunazidi kuishia,
Watalamu wa TEHAMA, pongezi zifike kwenu.
Kila mtu tunaona, viswaswadu vyaishia,
Simu janja twaziona, wengi zidi zitumia,
Huduma nyingi twaona, mikononi zaishia,
Watalamu wa TEHAMA, pongezi zifike kwenu.
Walimu asante sana, hawa kutufundishia,
Kazi yao njema sana, ile wanatufanyia,

Bila wao shida sana, malengo kuyafikia,
Watalamu wa TEHAMA, pongezi zifike kwenu.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Watakiwa kusaidia kuleta ufanisi kazi

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

WADAU wa maendeleo nchini wametakiwa kufanya kazi kwa kuwagusa wananchi ili kusaidia kuleta ufanisi wanapotekeleza majukumu yao.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alitoa rai hiyo jana kwenye hafla ya kupokea gari kutoka Shirika la Maendeleo ya Watu wa Marekani (USAID) kwa lengo la kusaidia kitengo cha elimu ya afya kwa umma kuifikia jamii katika kuleta uelewa juu ya masuala ya afya nchini.

Alisema kuna haja kubwa ya wadau kuwa wabunifu katika kutekeleza majukumu yao ili kuwafikia wananchi na kuhakikisha jamii inasaidiwa kutatua kero za kiafya kwenye maeneo yao.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa USAID, Dk. Ify Udo, aliishukuru serikali kupitia Wizara ya Afya ambao ndio wenye jukumu la kulinda afya za wananchi na kuhakikisha afya zao ziko salama.

**Alisema kuna haja kubwa ya wadau kuwa wabunifu katika kutekeleza majukumu yao ili kuwafikia wananchi na kuhakikisha jamii inasaidiwa kutatua kero za kiafya kwenye maeneo yao.**

# Mbaroni tuhuma kutapeli wastaafu

Na Augusta Njoji, DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, limewakamata watu watano kwa tuhuma za kujihusisha na utapeli dhidi ya wastaafu huku likiweka wazi mbinu zinazotumika kupata taarifa za wastaafu.

Miongoni mwa mbinu hizo ni kupiga simu kwenye ofisi au taasisi za serikali kujifanya watumishi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili wapatiwe taarifa za wastaafu.

Katika msako wa jeshi hilo, watuhumiwa hao walikutwa na nyaraka nane za serikali zenye taarifa za wastaafu na namba zao za simu.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, waliokamatwa wote ni wakazi wa mkoa wa Mwanza ambao ni David Makali, Anania Maxmillian, Solomoni Hosea, Kusekwa Ogelea na Isaya Bakuzwa.

Alisema kwa wiki kadhaa, jeshi hilo limekuwa likifanya msako wa kuwakamata wanaowatapeli wastaafu ambao wamekuwa wakiwarubuni kwamba watawasaidia kupata mafao yao.

"Watu watano wanashikiliwa na jeshi hili na wamekuwa wakijihusisha na wizi wa mtandao na kutapeli wastaafu.

"Wamekuwa wakiwatapeli wastaafu kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwamo kukusanya taarifa za wastaafu na wanawapigia simu maofisa na watu wa idara mbalimbali za serikali wakijifanya wao ni watumishi wa TAMISEMI au wakurugenzi wa ofisi hiyo na kuomba taarifa za wastaafu," alisema.

Alibainisha kuwa watuhumia hao wa utapeli wamekuwa wakisajili laini bandia za simu na kuwapigia wastaafu na kudai fedha ili kuwasaidia kulipwa madai yao kwa haraka au mapunjo yao.

Kamanda Otieno alitaja vitu vingine walivyokamatwa navyo ambavyo vimekuwa vikitumika kuwatapeli wastaafu kuwa ni mashine saba aina ya Famaco zinazotumika kusajili laini za kampuni zote za simu na zimeingiliwa na kuharibiwa mfumo wote elekezi wa usajili wa laini.

"Hizi mashine zinatumika kusajili laini za Vodacom lakini wao wamebutua zina uwezo wa kusajili laini yoyote iwe Airtel, Tigo, yaani ya aina yoyote ile. Mtu akienda pale anaulizwa unataka usajili moja kwa moja au ya uhalifu, kama ni ya uhalifu kuna majina mawaita. Tumewakamata mawakala pia wanne kwa hiyo wanaita unataka famba au takeaway.

"Pia tumewakuta na laini za simu 103 zilizosajiliwa na zinazotumika kwa uhalifu na laini 168 ambazo hazijasajiliwa. Lakini pia tumewakuta na vitambulisho vya watu mbalimbali na tumewakuta na simu 11 wanazotumia kwa mawasiliano maalum na watu waliowaweka kwenye mtego kwa ajili ya kuwatapeli," alisema.

"Hii moja ya nyaraka hapa unaiona ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo na hii ni orodha ya watumishi waliostaafu kuanzia Januari 2020 hadi Desemba 2021. Ukiangalia unaona kuna majina yamewekewa tiki ambayo tayari wastaafu wameshawasiliana nao na wameingia kwenye mtego wa kuwapa matapeli fedha.

"Hapa hii ya Wilaya ya Babati unaona hapa vyeo vimeandikwa kuna Inspekta, Sajenti na waliopigwa tiki wamefanya nao mawasiliano kuwaomba fedha," alisema huku akionyesha nyaraka hizo.

Alisema watuhumiwa hao bado wanashikiliwa na upelelezi unaendelea ili kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Mmoja wa watuhumiwa hao, David Makali, akizungumza kwa hiari bila kulazimishwa na polisi, alisimulia alichokuwa akifanya kuwa ni kupata taarifa kutoka kwa maofisa utumishi wa halmashauri husika na alikuwa akipiga simu akijifanya ni ofisa wa TAMISEMI.

"Nilikuwa napiga simu kama ofisa wa TAMISEMI, nilikuwa naomba taarifa za wastaafu. Kulingana na udhaifu wa watumishi ulivyo, wanaweza kukubali unatengeneza fomati anakupa taarifa na baadaye unageuka unakuwa kama mtu wa PSSSF unapiga simu kwa mstaafu," alisema.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, akiwa pamoja na maaskofu wa Kanisa la Angalikan Tanzania baada ya kufanyika ibada ya kumsimika Askofu wa Dayosisi ya Mpwapwa iliyofanyika jana, (kulia mwenye fimbo) Askofu Mkuu wa Kanisa la Angalikani Tanzania, Mahumbo Mdolwa. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Waziri ataka viongozi dini, siasa kuacha kudharau watangulizi wao

Na Paul Mabeja, MPWAPWA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, amewataka viongozi wa dini na siasa kuacha tabia ya kutoheshimu kazi ambazo zimefanywa na watangulizi wao.

Simbachawene alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza kwenye ibada ya kumweka wakfu Askofu wa Tatu wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Mpwapwa, George Chiteto.

"Iko kasumba kuwa askofu au waziri akiingia kwenye ofisi kila alichokifanya mwenzako unaona hakifai hata kile kizuri unataka kiwe chako. Hicho ni kinyume cha upendo wa Mungu," alisema.

Pia alisema serikali inatambua mchango wa makanisa nchini katika kuimarisha ustawi wa jamii.

"Tunatambua sana kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanywa na Kanisa la Anglikana Tanzania kabla ya uhuru na baada ya uhuru na sisi serikali tutaendelea kutoa ushirikiano kwenu, ninyi ndio wenye jukumu la kuimarisha ustawi wa jamii kwa kuwabadilisha watu kuwa wema tofauti na sisi ni kukamata na kuweka ndani," alisema Simbachawene.

Pia alisema serikali inaendelea na mikakati yake ya kuendeleza miradi ya elimu, afya, maji na kukamilika kwa wakati ili kutoa huduma kwa wananchi.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Kazi Maalum, George Mkuchika, alilipongeza kanisa hilo kwa kuendelea kufuata taratibu na katiba ya kanisa.

"Niwapongeze kwa kuendelea kufuata taratibu na katiba za kanisa kwa kupokezana uongozi. Leo hii nafasi hii kama msingekuwa mnafuata katiba yetu, tungesikia kwenye magazeti kanisa lina mgogoro jambo ambalo ni aibu kwa sisi Waanglikana," alisema Mkuchika.

Kwa upande wake, Askofu Chiteto, alisema uchaguzi umekwisha hivyo makundi yaliyokuwapo yamefutwa rasmi.

"Naombeni ushirikiano uchaguzi umekwisha na mimi ndiye Askofu. Nitakwenda kufanya kazi kwa ushirikianao, umoja ili kazi ya Mungu iende na kutimiza kusudi lake. Kila mmoja afanye wajibu wake bila kusukumwa. Mimi nitahudumia watu wote bila kubagua," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya nyumba ya maaskofu ya kanisa hilo, Askofu Dk. Dickson Chilongani wa Dayosisi ya Central Tanganyika, alisema wanampongeza Askofu Choteto kwa hatua aliyoifikia na wataendelea kumpa ushirikiano kila wakati.





# Ugonjwa Hemophilia waelezwa kuwa tishio

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TATIZO la upungufu wa chembechembe zinazosaidia damu kuganda (Hemophilia), limetajwa kuwa kubwa nchini huku wagonjwa wengi wakiwa bado hawajaibuliwa kutokana na kutofahamika.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipomwakilisha Mganga Mkuu wa Serikali kwenye uzinduzi wa kliniki ya ugonjwa huo katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Dk. Manyata alisema Tanzania inakadiriwa kuwa kuna wagonjwa wanaougua hemophilia kati ya 9,000 na 12,000, lakini waliotambuliwa na kuendelea na matibabu ni 172 pekee hali ambayo inahatarisha maisha ya ambao hawajatambuliwa.

Alisema ugonjwa huo ni tatizo duniani kwa kuwa mpaka sasa asilimia 97 ya wagonjwa duniani kote bado hawajatambuliwa kutokana na viashiria vyake kutofahamika mapema.

"Kwa Tanzania inaonyesha kwamba asilimia 99 ya wagonjwa wote bado hawajaibuliwa, sasa tuna kazi kubwa ya kuhakikisha hawa watu wanaibuliwa na kutibiwa ili kumaliza tatizo hili," alisema Dk. Manyatta.

Rais wa Chama cha Hemophilia nchini, Dk. Stella Rwezaula, alisema ugonjwa huo ni miongoni mwa magonjwa ya kurithi ambayo dalili zake huanza kuonekana kuanzia mtoto anapozaliwa.

Alisema kukosekana kwa chembechembe hizo zinazosaidia damu kuganda, kunasababisha mtu kutokwa na damu nyingi bila kukoma anapokuwa amepata jeraha la aina yoyote na hali hiyo huwa ni hatari.

Baadhi ya wagonjwa huwa wanatokwa na damu muda mrefu hata kama hawajapata jeraha na kusababisha kupoteza damu nyingi mwilini.

"Dalili za ugonjwa huu huanza kuonekana tangu utotoni kwa sababu anazaliwa akiwa na matatizo kwenye vina saba, tatizo lipo nchini kwetu na ni kubwa sana," alisema Dk. Stella.

Mmoja wa watu waliowahi kuugua ugonjwa huo, Abdulsadick Mhina, alisema mwanzoni ilikuwa vigumu kujitambua aina ya ugonjwa uliokuwa unamsumbua mpaka alipokwenda hospitalini kutibiwa na kuambiwa kuwa ni hemophilia.

Alisema alikuwa wakati mwingine anaamka asubuhi anakuta damu zinamtoka kwenye fizi ama magoti yamevimba au viungo vingine vya mwili ikiwamo mikono lakini alikuwa haelewi chanzo ni nini.

Awali wazazi wake walikuwa wanamweleza kuwa alikuwa na tatizo la upungufu wa chembechembe nyekundu za damu.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji aliwaomba Watanzania kuwasaidia watu wanaougua magonjwa ya aina hiyo kwa kuwa gaharama zake ni kubwa.

Alisema baadhi ya wagonjwa wanachelewa kutambua magonjwa yanayowasumbua kutokana na kukosa fedha za matibabu.

Aliviomba vyombo vya habari kusaidia kuhamasisha wananchi kupima afya zao ili kubaini matatizo yanayowasumbua na kutibiwa mapema.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Vijana, Kazi na Watu wenye ulemavu, Patrobas Katambi, akikagua viatu vinavyotengenezwa na kikundi cha wajasiriamali wenye ulemavu cha Mbalizi alipofanya ziara mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## 'Wananchi wote Mbeya watahesabiwa'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MRATIBU wa Sensa ya Watu na Makazi wa Mkoa wa Mbeya, Juma Maduhu amesema watahakikisha wananchi wote wa mkoa huo wanafikiwa na kuhesabiwa ndani ya muda uliopangwa.

Maduhu aliyasema hayo jana alipozungumza na gazeti hili kuhusu mwenendo wa sensa na kusema maeneo mengi yameshafikiwa na wananchi wamehesabiwa na kwamba yaliyobaki wameyaongezea nguvu.

Alisema makarani kila mmoja kwenye eneo alilopangiwa wanaendelea na kazi na waliomaliza wanahamishiwa kwenye maeneo yaliyobaki ili kazi imalizike haraka.

Alisema tangu shughuli ilipoanza mpaka sasa hakuna tatizo lililojitokeza la kukwamisha zoezi hilo kuendelea na hali ikiendelea hivyo itakamilika leo kama ratiba inavyosema.

"Tunawaomba wananchi ambao bado hawajafikiwa waendelee kuwa wavumilivu, makarani watawafikia maana kwa sasa mbinu tunayoitumia ni kuwahamisha makarani waliomaliza kazi kwenye maeneo yao kuwapeleka kwenye maeneo yaliyobaki ili washambulie haraka," alisema Maduhu.

Alisema kwa sasa wanaendelea kufuatilia na kubaini maeneo ambayo wananchi wengi hawajafikiwa ili kuongeza nguvu kwa kuwapeleka mawakala ambao wamemaliza kazi kwenye maeneo yao.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka viongozi wa Serikali za Mitaa kuhakikisha wanawaongoza makarani na wasimamizi wa sensa kwenye maeneo yao ili wananchi wote wafikiwe na kuhesabiwa.

Homera alisema hawatarajii mtu yeyote kurukwa kwenye zoezi hilo huku akiwataka wananchi ambao hawajafikiwa kuendelea kuwasubiri makarani mpaka wafikiwe.

# Wajasiriamali wenye ulemavu wapigiwa debe kusaidiwa masoko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imewaagiza maofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri zote nchini kuvisaidia vikundi vya wajasiriamali wenye ulemavu vinavyonufaika na mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya halmashauri kupata masoko ya bidhaa wanazozalisha

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Vijana, Kazi, na Watu wenye ulemavu, Patrobas Katambi, alisema hayo alipotembelea kikundi cha wajasiriamali wenye ulamavu wanaotengeneza viatu na kushona nguo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Katambi alisema vikundi hivyo vinanufaika na mikopo hiyo, lakini kutokana na kukosa masoko ya bidhaa zao wakati mwingine vinashindwa kurejesha mikopo hiyo kwa mujibu wa sheria.

Alisema maofisa maendeleo ya jamii wanaweza wakaandaa utaratibu wa kuwasaidia kwa kuwaandalia maandiko yatakayowawezesha kupata masoko kwenye taasisi mbalimbali za umma zikiwamo shule.

"Hawa watu wanazalisha bidhaa nzuri sana na wanaziuza kwa bei ya kawaida sana, sasa ni wajibu wenu maofisa maendeleo ya jamii kuwasaidia kupata masoko ambayo yatawasaidia kuinua biashara zao," alisema Katambi.

Vilevile, aliwataka maofisa hao kuwasaidia watu wenye ulemavu kunufaika na utaratibu wa asilimia mbili ya tenda za halmashauri ambayo ipo kwa mujibu wa sheria.

Mmoja wa wajasiriamali hao wenye ulemavu, Joseph Mwalongo, ambaye ni mwenyekiti wao alisema kikundi chao kinajishughulisha na kazi mbalimbali za uzalishaji ikiwamo za ushonaji.

Alisema yeye na kikundi chake wanashona na kuunda viatu wengine wanazalisha mafuta ya alizeti, wengine wanashona nguo na wengine wanafyatua na kuuza matofali katika mji huo wa Mbalizi.

Alisema ili kuendeleza shughuli zao waliomba mkopo wa Sh. milioni 38 kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na wakapatiwa kisha wakagawana kutokana na kila mmoja kuwa na shughuli zake.

"Mpaka sasa tunaendelea kurejesha mkopo na tumesharejesha zaidi ya Sh. milioni 20 na tunaendelea kurejesha, tunaishukuru serikali kwa kutusaidia mkopo huu ambao masharti yake ni nafuu sana umetusaidia kukuza shughuli zetu," alisema Mwalongo.

Alisema tatizo linalowakabili kwa sasa ni ukosefu wa masoko ya uhakika ya bidhaa wanazozalisha pamoja na ukosefu wa malighafi za uhakika na hivyo akaiomba Serikali kuendelea kuwasaidia kuzipata hasa malighafi za kuzalisha mafuta ya alizeti.

Alimwomba Naibu Waziri kuwasaidia kupata zabuni za kusambaza bidhaa zao kwenye taasisi mbalimbali za serikali ikiwamo shule na taasisi za kifedha kwa ajili ya kuuza nguo na viatu.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Madawa Bwana, alisema ofisi yake huvitembelea vikundi hivyo mara kwa mara kwa ajili ya kuangalia matatizo yanayowakabili na kuyapatia ufumbuzi.





# Hali ya chanjo UVIKO – 19 bado chini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR iko nyuma katika kufikia asilimia 70 ya watu waliochanja chanjo ya UVIKO-19 ifikapo Desemba, mwaka huu, baada ya kufikia asilimia 35.10 hadi Agosti 19.

Hayo yalisemwa jana mjini Zanzibar na Meneja wa Elimu ya Afya kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Bakari Hamad Magawarawa, wakati akitoa mada katika mafunzo ya waandishi wa habari jinsi ya kuripoti habari za UVIKO-19. Mafunzo hayo yaliandaliwa na Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC) kwa kushirikiana na Shirika la Internews.

Alisema bado idadi ya waliochanja chanjo hiyo ni ndogo ikilinganishwa na malengo ya serikali kufikia asilimia 70 ifikapo Desemba mwaka huu, huku akibainisha kuwa hadi kufikia Agosti 19, watu waliochanja walikuwa 267,824.

Alisema kati ya watu hao 267,824 ya waliochanja, wanaume 114,090 sawa na asilimia 30.9 na wanawake 153,734 ambao ni asilimia 33.1 ya lengo. "Wilaya ya Mjini Unguja waliochanja ni watu 47,956 sawa na asilimia 35, Magharibi A Unguja 19,189 sawa na asilimia 18, Magharibi B Unguja 20,573 sawa na asilimia 18 na Kaskazini A Unguja 9,704 sawa na asilimia 14.

"Wilaya ya Kaskazini B Unguja waliochanja ni 13,407 sawa na asilimia 29, Kati Unguja 10,922 sawa na asilima 25 na wilaya ya Kusini Unguja ni 10,219 ambao ni asilimia 45," alisema Magarawa.

Kwa upande wa Pemba, alisema Micheweni ndiyo wilaya inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watu waliochanja kuliko wilaya zote za Zanzibar baada ya watu 23,836 sawa na asilimia 44 kuchanja. Alisema Wilaya ya Mkoani Pemba waliochanja ni 11,674 sawa na asilimia 22, Wete 14,079 sawa na asilimia 24.

Meneja huyo aliwapongeza waandishi wa habari kwa kuwa na zaidi ya asilimia 90 ya waliopata chanjo na wamekuwa na mchango mkubwa katika jamii katika kuhakikisha inaongeza uelewa na kusaidia kupunguza kasi ya maambukizo ya ugonjwa huo.

Magarawa pia alisema bado ugonjwa wa UVIKO- 19 upo na Zanzibar inaendelea kupokea wagonjwa na kwamba Julai, mwaka huu, ilikuwa na wagonjwa watano.

Alisema waliopata ugonjwa huo wako waliochanja na ambao hawajachanja lakini nafuu ipo kwa waliochanja ambao hawakupata madhara makubwa ikilinganishwa na waliokuwa hawajachanja.

Magarawa aliwataka wananchi kuchanja chanjo hiyo hasa wenye magonjwa sugu kwa sababu ni waathirika wakuu wa kupata maradhi hayo pamoja na wenye umri mkubwa.

Akiwasilisha mada ya uandishi wa habari za UVIKO- 19 na chanjo dhidi ya ugonjwa huo, Mkuu wa Idara ya Mafunzo ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma Zanzibar ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Imane Duwe, aliwataka waandishi kuchukua tahadhari wanapokuwa katika majukumu yao ili wajikinge na maradhi hayo. Duwe aliwasisitiza waandishi wa habari kuzingatia maadili na kuhakikisha taarifa zinahusu wagonjwa na ugonjwa huo na kuzifanyie uchunguzi, lakini kuziwasilisha kwa kutumia lugha nyepesi kuepusha upotoshaji kwa umma.

Naye mwanasheria na mwandishi wa habari mwandamizi wa Shirika la Magazeti ya Serikali, Juma Khamis Juma, alisema ugonjwa wa UVIKO - 19 uliathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa habari na uhuru wa kujieleza.

Akiwasilisha mada katika mafunzo hayo, alisema hali hiyo ilisababisha waandishi wa habari kufanya kazi katika mazingira magumu na wakati mwingine kunyimwa taarifa muhimu zinazohusiana na ugonjwa huo.

Akifunga mafunzo hayo, Mwenyekiti wa ZPC, Abdalla Abdulrahman Mfaume, aliwataka waandishi kuyatumia mafunzo hayo kuleta tija katika kazi zao.

## SMZ yasisitiza ushirikiano na wadau maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, amesema serikali itaendelea kushirikiana na mashirika ya maendeleo ili kuimarisha sekta ya afya nchini.

Akizungumza jana na washirika wa maendeleo ya afya , ofisini kwake Mnazi Mmoja mjini Unguja baada ya kujadili masuala mbalimbali yanayohusu wahudumu wa afya ya kujitolea (CHV), alisema wahudumu hao ni muhimu na wanaisaidia wizara katika kuendesha harakati mbalimbali za kiafya.

Alisema wahudumu wa afya wa kujitolea wanafanya kazi ngumu na kubwa katika jamii ikiwamo kuwapatia elimu ya kuimarisha afya ya mama na mtoto jambo linaloisaidia wizara katika kupunguza madhara yatokanayo na uzazi.

Pia alisema wizara imejipanga kuhakikisha kuwa inaimarisha maslahi ya wahudumu hao ili kuwapa moyo zaidi wa kuendelea kufanya kazi na kuhakikisha afya za jamii zinaimarika.

"Baadhi ya wanajamii hawana uwelewa kuhusu maendeleo ya afya ya uzazi ambapo mama mjamzito huchelewa kufika hospitalini na kusababisha ongezeko la vifo vya mama na mtoto, hivyo wahudumu hawa wana jukumu kubwa la kutoa elimu zaidi kwa jamii," alisema Mazrui.

Kwa upande wao wajumbe wa shirika la D Tree, waliishukuru Wizara ya Afya kwa ushirikiano wao na kuahidi kuongeza ushirikiano zaidi katika sekta hiyo ili kupambana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza.

Wakati huo huo, Waziri Mazrui alikutana na ujumbe kutoka Uturuki na kujadili kuhusu upatikanaji wa dawa na vifaa tiba ambavyo vitasaidia katika matibabu mbalimbali kwa wagonjwa.



Baadhi ya waandishi wa habari walioshiriki mafunzo kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19 na chanjo ya ugonjwa huo yaliyoandaliwa na klabu ya waandishi wa habari Zanzibar (ZPC) kwa kushirikiana na Shirika la Internews, wakifuatilia uwasilishaji mada. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Zanzibar mguu sawa magari ya gesi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema Zanzibar iko tayari kuanza matumzi ya magari yanayotumia gesi asilia.

Aliyasema hayo jana alipokutana na kampuni inayojishughulisha na utengenezaji wa magari yanayotumia gesi na ujenzi wa miundombinu ya barabara ya 360 ECO Group kutoka Australia yenye nia ya kuja kuwekeza nchini, ofisini kwake Mwanakwerekwe, Unguja.

Mbali na kutaka kuwekeza katika masuala ya usafirishaji, kampuni hiyo pia inatarajia kujenga vituo vya utoaji wa mafunzo ya usalama barabarani na namna ya bora ya matumizi ya magari yanayotumia gesi.

Alisema serikali ya Zanzibar inaendelea na mchakato wa uchunguzi na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia ambazo hivyo kwa sasa zimekuwa na gharama kubwa, hivyo ni wakati mwafaka wa kukaa na kampuni hiyo kuona ni kwa namna gani inaweza kusaidia matumizi ya magari yanayotumia gesi asilia.

Waziri Soraga alisema matumizi ya gesi yatapunguza gharama zaidi kuliko gharama zinazotumika kwenye magari yanayotumia mafuta ya petroli na dizeli jambo ambalo litawasaidia wananchi kuwapunguzia gharama za maisha.

"Tuzungumze na washirika wa jambo ndani ya serikali ili lifanikiwe kwa urahisi na lianze kuwasaidia wananchi wetu lengo letu na kurahisisha maisha ya wananchi," alisema Soraga.

Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya Kazi na Uwezeshaji, Dk. Islam Seif Salim, aliishauri kampuni hiyo kutoa mabasi yanayotumia gesi na mafunzo ya matumizi ya magari hayo kwa madereva wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA) ili kuona ubora wa matumizi ya gari hizo.

Mkurugenzi Mkuu wa 360 ECO Group, Johann Rieger, alisema nia yao ni kuisaidia serikali na inakuwa nchi ya mfano katika usafirishaji kutokana na udogo wa eneo na urahisi wa ujenzi wa miundombinu.

Alisema atahakikisha wanatoa mabasi yanayotumia gesi asilia yenye ubora wa kimataifa pamoja na kutoa mafunzo ya matumizi ya gari pamoja na kuzalisha ajira kwa vijana wa Zanzibar.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## CHAMA CHA WAKULIMA NA WAFUGAJI - LWANJILI GROUP S. L. P 70, CHIMALA - MBARALI - MBEYA

**CHAMA KINAWATAFUTA HAWA WAFUATAO**

1. **Jonisia Berenadi Muhando**
2. **Allen Kwiyeli Ngailo**
3. **Rajabu Rashid Ghuliku**
4. **Bahati Mennath Mwahalende**
5. **Davice Hilmar Msanga**
6. **Emmanuel Lukas Silumba**

IMETOLEWA NA MWENYEKITI WA CHAMA

ADAM M. MALEMA

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAGRETH CLEMENCE NGUSSA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0359-0067** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **KIGURUNYEMBE** mwaka 2019,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi control number : **9910834007171**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIAM ANGETILE HIDA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya **TRAILER** yenye namba za usajili **T 264 AWG.**

Chasis Namba: **A222730**

Kadi Namba: **6246657**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi, taarifa ya polisi RB namba

**DSM/PHQ/RB/315060/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NA.43/2022**
**(Arising from land case NO. 3/2022)**

**HUSSEIN ABDALLAH KANIKI AND ANOTHER.........1ST MDAI**
**EMMANUEL KURES LOVOYO.......2ND MDAI**
**VERSUS**
**ATHUMAN HOKORORO..................1ST MDAIWA**
**ERNEST LUYANGI...............2ND MDAIWA**
**M/S STANA BROTHERS (MOHAMED HUSSEIN DEWJI)..................3RD MDAIWA**
**M/S SPEED SECURITY SERVICE LTD (IMRAN MOHAMED DEWJI).................4TH MDAIWA**

**Kwa:**

- **ATHUMAN HOKORORO**
- **ERNEST LUYANGI**
- **M/S STHANA BROTHERS ( MOHAMED HUSSEIN DEWJI)**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Wadai tajwa hapo juu wamefungua shauri la utekelezaji dhidi yenu mnatakiwa kufika katika mahakama hii tukufu wewe mwenyewe au wakili wenu anayetambulika kisheria **tarehe 12/09/2022 saa 4:00** asubuhi kujibu madai dhidi yenu.

Mnaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo mnataraji kuvitumia katika utetezi wenu siku hiyo.

**KUMBUKA KUWA:** Msipohudhuria siku hiyo na mahakama ikithibitisha kama mmepokea wito huu, mahakama itaamuru utekelezaji kuendelea.

**Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo tarehe 15 mwezi Agosti, 2022.**

NAIBU MSAJILI
KANDA YA DAR ES SALAAM

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......46/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HAMISI SESEMU WA SABASABA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**YALIYOLETWA NA SAID HAMISI SESEMU**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 26 Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 11 mwezi 08 mwaka 2022**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

HAKIMU MFAWIDHI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FATOUMATA KABORE LANKWANDE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **HONDA FIT** yenye usajili namba **T20DC 464, CHASSIS NAMBA: GG73007817** na **ENGINE NAMBA: L15A7009298.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/338224/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAINESS ISRAEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0219-0038** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **SONGEA GIRLS** mwaka **2002**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi taarifa **SAM/B.I/24/VOL.14/133**

---

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**
**Kumb Na. IMC/L/32043/15/IHK 30/08/2022**
**Kwa yeyote anayehusika,**

**SHERIA YA USAJILI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO PAMOJA NA**
**STAKABADHI ZA MALIPO YA KIWANJA.**

**Barua ya Toleo (Letter of Offer) ya Kiwanja pamoja na stakabadhi za malipo ya kodi ya Kiwanja (New Offer Charges & Land Rent receipts), Kiwanja Na 1322 Kitalu 'A' NYASAKA.**

Mmiliki aliyeandikishwa: **JOHN BOSCO wa S.L.P 1760, Mwanza.**
Muombaji: **JOHN BOSCO wa S.L.P 1760, Mwanza.**
Ardhi: **Kiwanja Na. 1322 kitalu 'A' NYASAKA, Manispaa ya Ilemela**

**TAARIFA IMETOLEWA** kwamba Barua ya Toleo (Letter of Offer) ya Kiwanja pamoja na stakabathi za malipo ya kodi ya kiwanja ya kumiliki ardhi (New Offer charges &Land Rent receipts) vilivyotajwa hapo juu vimepotea na ninakusudia kutoa Nakala halisi ya Barua ya Toleo(Letter of Offer) ya kiwanja pamoja na stakabadhi zote za malipo ya kodi ya kiwanja badala yake iwapo hakuna kipingamizi chochote kitakachojitokeza ndani ya muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii.

Barua ya Toleo (Letter of Offer) ya Kiwanja pamoja na stakabadhi za malipo ya kodi ya kiwanja (New Offer charges &Land Rent receipts) halisi vikionekana virudishwe Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.

I.H.Kalogne,
Kny: MKURUGENZI WA MANISPAA,
MANISPAA YA ILEMELA.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NURU ALLY KAMCHAPE** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 862 CXL** aina ya **TVS,** yenye Chasis No. **N5040800**, Engine No. **AF7BM1906622**. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**Taarifa ya polisi MWA/NY/RB/340649/2022.**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni IndustRial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# IAEA kutembelea kituo cha nyuklia Ukraine

**KYIV, UKRAINE**

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Nishati ya Atomiki (IAEA), amesema ujumbe wa shirika hilo uko njiani kuelekea kwenye kinu cha nyuklia cha Zaporizhia ambacho kinahofiwa kuweza kusababisha maafa baada ya kuharibiwa nchini Ukraine.

Kinu hicho cha nyuklia kililengwa na mashambulizi yaliyofanyika wiki chache zilizopita, hali iliyotia hofu ya kutokea kwa ajali kubwa.

Alisema, ujumbe huo wenye watu 10 utawasili kwenye eneo hilo ndani ya wiki hii. "Siku imewadia, ujumbe wa IAEA, kwenda Zaporizhia sasa uko njiani, ni lazima tulinde usalama wa Ukraine na mtambo mkubwa zaidi wa kuzalisha umeme barani Ulaya," alisema.

Pia, ilielezwa kuwa Grossi aliomba kwa miezi kadhaa kuweza kwenda kwenye eneo la tukio, akionya juu ya hatari halisi ya maafa ya nyuklia katika Kiwanda cha Zaporizhia, ambapo kunapatikana vinu sita kati ya 15 vya Ukraine.

Taarifa ya RFI, ilisema kinu hicho kilidhibitiwa na wanajeshi wa Urusi mwezi Machi baada ya uvamizi dhidi ya Ukraine kuanza Februari 24, na kwamba kiko karibu na uwanja wa mapigano kusini mwa Ukraine.

Taarifa zilieleza kuwa mji mkuu wa Ukraine Kyiv na wa Urusi Moscow wanatuhumiana kila mmoja kwa kufanya mashambulizi karibu na kituo hicho cha nyuklia, karibu na mji wa Energodar, kwenye Mto Dnieper, na kusababisha kinu hicho kuwa kwenye hatari.

Siku ya Jumamosi shirika la taifa la nishati ya nyuklia la Ukraine, Energoatom, lilionya juu ya hatari ya uvujaji wa mionzi na moto baada ya mashambuizi mapya, na kwamba katika wiki za karibuni, nchi za magharibi zilitiwa wasiwasi na hali inayojiri karibu na kinu cha Zaporijgia.

Pia, Umoja wa Mataifa (UN) ulitoa wito wa kukomeshwa kwa shughuli zote za kijeshi katika eneo lililokaribu na kituo hicho cha nyuklia.

Vilevile ilielezwa kuwa awali Ukraine ilihofia kuwa ziara kama hiyo ingehalalisha uvamizi wa Urusi kwenye kituo hicho mbele ya jumuiya ya kimataifa kabla na hatimaye kuunga mkono wazo la ujumbe wa IAEA.

Akikabiliwa na hali hii hatari Rais Volodymyr Zelensky, aliwahimiza maofisa wa nyuklia wa UN siku ya Ijumaa kutuma timu haraka iwezekanavyo.

"Kati ya Alhamisi na Ijumaa, mtambo huo na vinu vyake sita vya megawati 1,000 kila kimoja vilitenganishwa kabisa na gridi ya taifa kutokana na kuharibika kwa njia za umeme, kulingana na Kyiv, kabla ya kuunganishwa na kuwashwa upya," ilisema.

Ofisi ya rais wa Ufaransa ilionyesha katikati ya mwezi Agosti baada ya kufanyika mahojiano ya simu, kwamba Vladimir Putin alikubali ujumbe huo kwenda Ukraine na sio Urusi, madai ambayo ilikuwa imeyatoa awali.

***RFI***

# 10 wauawa machafuko DRC

**ITURU, DRC**

VYANZO vya kijeshi vya mashariki mwa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), vimesema zaidi ya watu 10 wameuawa akiwamo mwanajeshi mmoja kutokana na machafuko yaliyodumu kwa siku tatu katika jimbo la Ituru.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA, zaidi ya makundi ya wanamgambo 120 yamesambaa mashariki mwa DRC, huku ikielezwa kuwa kumekuwa na mashambulizi ya mara kwa mara dhidi ya wakazi wa eneo husika.

Kiongozi wa kijeshi katika jimbo la Kivu Kaskazini alisema wamempoteza mwanajeshi shujaa katika shambulio dhidi ya ngome yao katika kitongoji cha kaskazini mwa mji wa Butembo, lililofanywa na wanamgambo wa Mai-Mai.

Kiongozi huyo ambaye hakutaka jina lake litajwe, alisema wanamgambo wawili wa kundi hilo pia waliuawa kutokana na ghasia hizo.

Kiongozi wa shirika la kiraia huko Lodjo, katika jimbo la Kaskazini Mashariki la Ituri Prince Kaleta, alibainisha kuwa wachimba dhahabu sita waliuawa Jumapili na kukatwa vichwa na waasi wa kundi la CODECO, ambalo ni kisasa na kidini na inaelezwa kuwa linawakilisha maslahi ya watu kutoka kabila la Lendu.

"Kundi hilo linachukuliwa kama moja ya makundi ya wanamgambo yanayofanya ukatili, na linashtumiwa kwa mauaji ya kikabila huko Ituri," taarifa ilisema.

Mkuu wa Mtaa katika eneo la utawala wa Bashi, wilaya ya Beni Flavien Kakule, pia alisema raia watatu waliuawa Jumamosi usiku katika shambulio lilofanywa na waasi wa kundi la ADF huko Kivu Kaskazini.

***VOA***



Mwananchi akichota maji katika kisima kilichoko eneo la Sukkur, moja ya sehemu zilizokumbwa na mafuriko. **PICHA: MTANDAO**

# Mafuriko Pakistan idadi ya vifo yaongezeka

**SUKKUR, PAKISTAN**

MAMLAKA ya Kitaifa ya Kukabiliana na Majanga (NDMA) imesema takribani watu 1,061 wameuawa nchini Pakistan kutokana na mafuriko ambayo yametokana na mvua zilizoanza kunyesha mwezi Juni mwaka huu na kusababisha taifa hilo kukumbwa na maafa makubwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na RFI, serikali nchini humo ilitangaza hali ya hatari Agosti 26 huku mvua ikiendelea kunyesha, na kwamba zaidi ya wakazi milioni 33, au mkazi mmoja kati ya saba wameathiriwa na mafuriko hayo.

Taarifa zilieleza kuwa mojawapo ya majimbo yaliyoathirika zaidi ni Sindh kusini mwa nchi hiyo.

"Macho yanaelekezwa kwenye bwawa la Sukkur, kwa sababu ni juu yake kwamba kunategemewa hatima ya maelfu ya watu kusini mwa Pakistan, hifadhi hii ya maji ni msingi wa mfumo wa umwagiliaji nchini humo pia ni mtandao mkubwa wa umwagiliaji wa aina hii duniani," ilisema taarifa.

Pia, ilielezwa kuwa ni hatari kwa mto huo ambao hutoa asilimia 90 ya maji ya nchini Pakistan, na kwamba hujaa maji na kusababisha mafuriko katika vijiji vyote vinavyozunguka bwawa hilo.

"Vijiji vingi tayari vimesombwa na maji, kumeonekana mashamba makubwa ya kilimo, bustani ya miembe na mitende, yakizamishwa chini ya maji na maelfu ya watu walionusurika wakiwa wamekusanyika chini ya mahema ya muda pembezoni mwa barabara," ilisema.

Aidha, iliongeza kuwa waokoaji wanakabiliwa na kazi ngumu usiku na mchana kusaidia wakazi walionaswa, pamoja na kuwaletea chakula wale wanaokataa kuondoka makwao licha ya hatari ya kipindi kipya cha mvua kubwa, huku wakazi wa eneo hilo wakijikita kwenye maombi ili mvua hizo ziache kunyesha.

***RFI***

# TEMBO WARRIORS, SERENGETI GIRLS KAMBINI UTURUKI, UINGEREZA

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu (Tembo Warriors) na Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya umri wa miaka 17 (Serengeti Girls), zinatarajia kuondoka nchini mapema mwezi ujao kuelekea nchini Uturuki na Uingereza kuweka kambi kwa ajili ya kujiandaa na Fainali za Kombe la Dunia, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana katika semina ya waandishi wa habari za michezo iliyoandaliwa na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, alisema Serengeti Girls itaelekea Uingereza kuweka kambi katika Kituo cha Klabu ya Southampton inayoshiriki Ligi Kuu England na kisha nchi moja ya Kiarabu kwa maandalizi zaidi kabla ya kwenda nchini India katika fainali hizo za Kombe la Dunia kwa Wanawake wenye umri chini ya miaka 17, zitakazofanyika Okotoba mwaka huu.

Alisema, Tembo Warriors ambayo nayo Oktoba mwaka huu itakuwa na kibarua kigumu cha kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kwenye Fainali za Kombe la Dunia kwa Watu wenye Ulemavu, yenyewe itaenda kuweka kambi Uturuki nchi ambayo fainali hizo zitafanyika.

Dk. Abbas, alisema serikali imeshaweka mikakati yao kwa timu hizo kwenda kuweka kambi katika mataifa hayo.

"Tunaandaa timu zetu za taifa kufanya vizuri katika mashindano hayo, Tembo Warriors wataenda Uturuki wiki mbili kuweka kambi, kucheza mechi za kirafiki kwa ajili ya kupata uzoefu na kuzoea mazingira.

"Kwa upande wa Serengeti Girls wataenda Kituo cha Southampton, tumechagua kwenda huko kwa sababu timu yetu itacheza mechi ya kirafiki na timu ya wanawake ya klabu hiyo," alisema Dk. Abbas.

Alisema, Serengeti Girls watakaa Uingereza wiki mbili na baadaye wataenda moja ya taifa la Kiarabu kwa ajili ya kuendelea na kambi yao kabla ya Oktoba mwaka huu.

"Malengo yetu (serikali) ni kuandaa timu zetu za taifa kuwa imara na kufanya vizuri kwenye mashindano yaliyopo mbele yetu, ikiwamo hayo ya Kombe la Dunia," alisema.

**KOKOTA...**



Mshambuliaji wa Taifa Stars, Danny Lyanga (kulia), akikokota mpira huku beki wa kulia wa Timu ya Taifa ya Uganda 'Uganda Cranes', Gavin Kizito, akipiga hesabu za kumdhibiti kwenye mechi ya mkondo wa kwanza kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Uganda ilishinda bao, 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Nkoma kuipika Simba Queens mpya ya CAF

**Na Hadija Mngwai**

BAADA ya kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa kwa Wanawake Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), uliowapa tiketi ya kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, amesema kazi aliyonayo kwa sasa ni kuhakikisha anatengeneza kikosi bora cha kwenda Morocco kwenye fainali hizo.

Simba Queens, imeweka rekodi Tanzania baada ya kuwa timu ya kwanza ya wanawake kwa ngazi ya klabu kukata tiketi ya kwenda kushiriki fainali hizo za Afrika zitakazofanyika nchini Morocco Oktoba mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe, Nkoma alisema, lengo lake ni kuona anaimarisha timu hiyo ili iweze kuwa bora zaidi itakapokwenda nchini Morocco kama alivyofanikisha malengo yake ya kutwaa ubingwa wa CECAFA.

"Nimeshukuru kutwaa ubingwa huu, kwa sasa ni mapema kuzungumzia mikakati ya timu, lakini nahitaji kukaa chini na uongozi ili kuwapa tunachokihitaji na mawazo yetu ili kuweza kutengeneza kikosi kilicho bora.

"Nahitaji kuwa na kikosi bora kitakachokwenda Morocco, hii si mara yangu ya kwanza kuchukua ubingwa, ni mara ya tatu, pia niliwahi kuchukua ubingwa wa Cecafa na Serengeti Boys ya Gabon na sasa haijulikani ilipo.

" Nitatengeneza Simba nyingine kabisa ya kuchukua ubingwa Morocco, kikubwa ni maandalizi," alisema Nkoma, ambaye katika michuano hiyo ya CECAFA, ameiongoza Simba Queens kumaliza kwa kushinda michezo yote.

# Mchengerwa aipongeza JWTZ kuleta medali madola

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, amesema Watanzania wanamwamko kwenye michezo kutokana na sapoti ya Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta hiyo.

Mchengerwa aliyasema hayo juzi alipokuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya kumuaga aliyekuwa Mkuu wa Majeshi, Jenerali Venance Mabeyo, ambaye alikuwa mlezi wa Klabu ya TPDF Lugalo, Dar es Salaam, na kumkaribisha Mkuu wa Mpya wa Majeshi Tanzania, Jenerali Jacob Mkunda.

Alisema, tangu mwaka 1982, Tanzania haijawahi kufanya vizuri kwenye mashindano ya Jumuiya ya Madola, lakini mwaka huu wachezaji wa jeshi wameitoa nchi kimasomaso kwa kufanikiwa kurudi na medali za ushindi.

Waziri huyo alisema Tanzania mwaka huu imefanikiwa kupata medali, huku akifafanua kuwa asilimia 99 ya wachezaji waliofanya vizuri wametoka kwenye timu za majeshi.

"Napenda kuchukua fursa hii kukupongeza Jacob Mkunda, kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Kwetu sisi wanamichezo ni faraja kubwa, tunaamini uzoefu wako kama mlezi wa wanamichezo ndani ya jeshi letu tutafanya vizuri zaidi, kwani nakiri kuwa Watanzania wamekuwa na mwamko kwenye michezo kutokana na kuungwa mkono na Rais wetu, Samia Suluhu Hasssan," alisema Mchengerwa.

Aidha, Mkuu wa Majeshi mpya, Jenerali Mkunda, alimpongeza Mkuu wa Majeshi mstaafu, Jenerali Mabeyo kwa kuendeleza klabu hiyo kuwa miongoni mwa klabu bora za gofu nchini, na kuahidi kuendelea kushirikiana na wanachama na uongozi wa klabu ya TPDF Lugalo kuhakikisha mchezo huo unazidi kukua.

Mwakilishi wa Benki ya NBC, Elbariki Masuke, alisema benki hiyo inaongoza kuidhamini michezo mbalimbali ikiwamo Ligi Kuu, huku akiahidi kuendelea kudhamini mashindano mengine yatakayoandaliwa na klabu hiyo.

"Tunadhamini michezo mbalimbali kama riadha, ambayo pesa zake tunazipeleka kusaidia matatizo ya saratani ya mlango wa kizazi upande wa wanawake, lakini pia tunatambua kuwa michezo ni ajira na imewasidia vijana wengi kupata ajira rasmi na zisizo rasmi," alisema Masuke.

Nahodha wa klabu hiyo, Japhet Masai, yeye alisema shindano hilo limeshirikisha wachezaji kutoka klabu zote nchini, ambapo washindi walipata zawadi mbalimbali, huku mshindi wa jumla akiwa William Mtweve, aliyepata zawadi ya kombe na nyinginezo.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### AUBAMEYANG NA CHELSEA

KLABU ya Chelsea imefufua nia yao ya kumnunua fowadi wa Crystal Palace na Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 29, lakini mshambuliaji wa Barcelona na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye miaka 33, anabakia kuwa kipaumbele chao cha kwanza. ***(Guardian)***

### RONALDO ATAFUTIWA SOKO

WAKALA wa mshambuliaji wa Manchester United na Ureno, Cristiano Ronaldo amerejea Chelsea akichunguza iwapo kuhamia Stamford Bridge kunawezekana kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37. ***(Independent)***

### ZIYECH AWANIWA AJAX

KLABU ya Ajax wanamlenga winga wa Chelsea na Morocco, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka wa 29, kuchukua nafasi ya Antony mwenye miaka 22, baada ya kukubali ofa kutoka kwa Manchester United kwa ajili ya kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil. ***(Mail)***

### BROJA ATAKIWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea imetoa ofa kwa mshambuliaji wa Everton na Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 20, na kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 22, pamoja na pauni milioni 25 ili kumnunua mshambuliaji wa England, Anthony Gordon, 21. ***(Football Insider)***

### DE JONG KUBAKI BARCA

KIUNGO wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, anatarajiwa kusalia Nou Camp msimu huu wa majira ya joto, licha ya Manchester United, Chelsea na Liverpool kumtaka. ***(CBS Sports)***

### CAVANI KUTUA VALENCIA

KLABU ya Valencia ina uhakika wa kuipiku Real Sociedad katika kumsajili Edinson Cavani, mwenye umri wa miaka 35, na wanatarajiwa kumpa mshambuliaji huyo wa Uruguay mkataba wa miaka miwili. ***(Fabrizio Romano)***

### BERGE KUNUNULIWA LIVER

KLABU ya Liverpool inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Sheffield United na Norway, Sander Berge mwenye umri wa miaka 24. ***(Yorkshire Post)***

### PEREIRA AGOMBEWA EPL

KLABU ya Leicester na Everton zinafikiria kumnunua mshambuliaji wa Al Hilal, raia wa Brazil, Matheus Pereira mwenye umri wa miaka 26. ***(Sun)***

### REGUILON ATAKIWA ATLETICO

MLINZI wa Tottenham Hotspur, na Hispania, Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 25, anatazamiwa kujiunga na Atletico Madrid kwa mkopo bila kipengele cha kumnunua jumla. ***(Fabrizio Romano)***

### WINKS ANUKIA SAMPDORIA

KIUNGO wa kati wa Tottenham Hotspur na England, Harry Winks mwenye umri wa miaka 26, anakaribia kuhamia Sampdoria. (Evening Standard)

### CHALOBAH HAONDOKI CHELSEA

CHELSEA, imeamua mlinzi wao, Trevoh Chalobah mwenye 23, hataondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto licha ya kufanya mazungumzo na Inter Milan, AC Milan na RB Leipzig kuhusu uwezekano wa mkataba wa mkopo. ***(Fabrizio Romano)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI: LEWANDOWSKI NI KIONGOZI WA ASILI

Mbali na mabao, anajua kuongoza vizuri sana uwanjani, kile anachokiona anasema...

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Xavi amemmiminia sifa nyingi "kiongozi wa asili" Robert Lewandowski, baada ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Real Valladolid, Jumapili.

Nyota huyo ambaye alisajiliwa kipindi cha majira ya joto kutoka Bayern Munich, alifunga mabao mawili katika mechi ya pili mfululizo na kumfanya afikishe mabao manne.

"Mbali na mabao, yeye ni kiongozi mzuri sana uwanjani," alisema Xavi akiiambia DAZN.

"Yeye ni kiongozi wa asili; kile anachokiona anasema. Inashangaza jinsi alivyozoea kundi hili haraka. Ni nyota aliyezaliwa kuwa mfano."

Wakiwa wameanza kampeni kwa sare tasa dhidi ya Rayo Vallecano, Barcelona wamepata ushindi wa pili mfululizo dhidi ya Real Sociedad na Real Valladolid, wakifunga mabao nane kwa ujumla.

Wakati xavi, aliweka wazi kuna maeneo ya kuboreshwa, alipongeza timu hiyo kwa uchezaji "wa ajabu".

"Hapana kabisa, lakini ilikuwa mechi nzuri. Dakika 40 za kwanza zilikuwa nzuri sana. Kisha tukapumzika. Sehemu ya pili tulianza vizuri pia," aliongeza.

"Kwa ujumla, ilikuwa mechi nzuri, lakini si kamili. Si lazima kupumzika na lazima uendelee kubana. "Hii ni nzuri kwa timu na kwa mashabiki. Hatupaswi kupumzika kama ilivyotokea kwa mabao 2-0, lazima niangalie mchezo unaofuata."

Mchezo unaofuata wa Barcelona ni dhidi ya Sevilla kabla ya kuanza kampeni ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakiwa wamepangwa kundi moja na Bayern Munich na Inter.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 327,

MECHI KALI

SOUTHAMPTON
VERSUS
CHELSEA

1 | 5.19
X | 4.09
2 | 1.56

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ANTONY MAMBO SAFI MAN UNITED



**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imefikia makubaliano na Ajax kwa ajili ya kumnunua winga wa Brazil, Antony.

Inafahamika kwamba, United watalipa ada ya awali ya pauni milioni 80.75 na nyongeza ya pauni milioni 4.25.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, anatarajiwa kuwasili Manchester kukamilisha uchunguzi wa afya ndani ya saa 48 zijazo kuanzia jana.

Antony atakuwa mchezaji wa pili kusajiliwa na Man United pamoja na beki Harry Maguire, baada ya Paul Pogba aliyesajiliwa kwa pauni milioni 89.

Antony, alifunga mabao 25 na kutoa asisti 22 katika mechi 82 alizoichezea Ajax, baada ya kujiunga nayo kutoka Sao Paulo mwaka 2020 na kucheza chini ya kocha wa sasa wa United, Erik ten Hag.

Alianza mechi yake ya kwanza ya kimataifa akiwa na Brazil Oktoba 2021 na ana mabao mawili katika mechi tisa.

Antony, ambaye alichangia mabao saba katika mechi zake 11 za Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Ajax, pia ni mchezaji wa nne aliyesajiliwa kwa gharama kubwa zaidi katika historia ya Ligi Kuu England.

# Pogba alengwa na kundi la kihalifu

**TURIN, Italia**



PAUL Pogba, amesema amekuwa akilengwa na wanyang'anyi na vitisho kutoka kwa genge la uhalifu wa kupangwa.

Kiungo huyo wa Juventus na Ufaransa alitoa taarifa kupitia kwa mawakili wake Jumapili akisema suala hilo limeripotiwa kwa mamlaka husika.

Shirika la Habari la AFP, likinukuu chanzo kimoja limesema Polisi wa Ufaransa wameanzisha uchunguzi.

Hapo awali, kaka yake Pogba, Mathias alichapisha video mtandaoni akiahidi kuchapisha "ufichuzi mkubwa" kuhusu mchezaji huyo.

"Ni pamoja na vitisho na majaribio ya unyang'anyi ya genge lililopangwa dhidi ya Paul Pogba," ilisema taarifa hiyo.

"Mashirika yenye uwezo nchini Italia na Ufaransa yalifahamishwa mwezi mmoja uliopita na hakukuwa na maoni zaidi kuhusiana na uchunguzi unaoendelea."

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa Ufaransa mwaka 2018, Pogba alihamia Juventus kwa uhamisho wa bure msimu huu baada ya kuondoka Manchester United.

Katika video zake, Matthias Pogba alisema "ulimwengu mzima, pamoja na mashabiki wa kaka yangu, na hata zaidi timu ya Ufaransa na Juventus, wachezaji wenzake na kaka yangu na wafadhili wake wanastahili kujua mambo fulani".

Alisema ufichuzi huo unamhusisha wakala wa Pogba, Rafaela Pimenta.

## HABARI MICHEZO


,973,700

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 31/08/22 | 19:30 | Empoli vs Verona | 2.61 | 3.26 | 2.56 |
| 02. 31/08/22 | 19:30 | Udinese vs Fiorentina | 2.86 | 3.36 | 2.31 |
| 03. 31/08/22 | 20:00 | Angers vs Reims | 2.42 | 3.21 | 2.86 |
| 04. 31/08/22 | 21:00 | Rostov vs Dinamo Moscow | 2.60 | 3.18 | 2.50 |
| 05. 31/08/22 | 22:00 | Farul Constanta vs Steaua Bucuresti | 2.84 | 3.09 | 2.47 |
| 06. 02/09/22 | 03:30 | Atletico GO vs Sao Paulo | 2.84 | 3.04 | 2.39 |
| 07. 02/09/22 | 13:30 | Incheon Utd vs Gangwon | 2.65 | 3.24 | 2.42 |
| 08. 02/09/22 | 13:30 | Consadole Sapporo vs Cerezo Osaka | 2.54 | 3.27 | 2.49 |
| 09. 02/09/22 | 19:30 | Heidenheim vs Fortuna Dusseldorf | 2.43 | 3.26 | 2.76 |
| 10. 02/09/22 | 21:00 | Mezokovesdi SE vs Zalaegerszegi TE | 2.47 | 3.36 | 2.52 |
| 11. 02/09/22 | 21:45 | Le Havre vs Caen | 2.53 | 3.08 | 2.78 |
| 12. 02/09/22 | 22:00 | West Bromwich vs Burnley | 2.41 | 3.11 | 2.91 |
| 13. 02/09/22 | 22:00 | Leganes vs Eibar | 2.59 | 2.84 | 2.93 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 30/08/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 5118 | Bucheon vs Gwangju | 3.48 | 3.18 | 2.01 |
| 16:30 | 2380 | CS Mioveni vs UTA Arad | 2.75 | 2.95 | 2.65 |
| 17:10 | 1466 | Umm-Salal SC vs Al Rayyan SC | 2.25 | 3.43 | 2.75 |
| 17:30 | 2973 | National Bank vs Enppi Club | 2.32 | 2.87 | 3.38 |
| 17:30 | 5431 | Atalanta Youth vs Roma Youth | 3.04 | 3.68 | 2.00 |
| 17:30 | 5681 | Smouha Club vs Farco FC | 2.18 | 2.80 | 3.85 |
| 18:30 | 1991 | Bohemians vs Ceske Budejovice | 2.02 | 3.56 | 3.51 |
| 18:30 | 2895 | Zlin vs Pardubice | 2.08 | 3.41 | 3.51 |
| 19:00 | 1656 | Admira Wacker vs SCR Altach | 3.68 | 3.53 | 1.83 |
| 19:00 | 1875 | Apollon Limassol vs EN Paralimni | 1.33 | 5.07 | 8.32 |
| 19:00 | 2062 | Spartak Moscow vs Kryliya Sovetov | 1.55 | 4.12 | 4.71 |
| 19:00 | 5115 | MFK Skalica vs MSK Zilina | 2.79 | 3.38 | 2.24 |
| 19:15 | 4289 | U Craiova SA vs Sepsi Osk | 2.90 | 3.15 | 2.40 |
| 19:30 | 4315 | Ismaily SC vs Talaea El Gaish | 3.07 | 2.77 | 2.57 |
| 19:30 | 5635 | Sassuolo vs AC Milan | 5.00 | 4.20 | 1.56 |
| 20:15 | 5865 | Bnei Sakhnin vs Maccabi Haifa | 6.27 | 4.22 | 1.42 |
| 20:30 | 2181 | SV Horn vs SKN St Polten | 3.14 | 3.39 | 2.05 |
| 21:00 | 2952 | Derby vs Grimsby | 1.73 | 3.58 | 4.12 |
| 21:00 | 4273 | Exeter vs Newport | 1.96 | 3.44 | 3.34 |
| 21:00 | 5842 | MK Dons vs Cheltenham | 1.85 | 3.49 | 3.68 |
| 21:30 | 1594 | Bradford City vs Sheffield Wed | 3.44 | 3.39 | 1.95 |
| 21:30 | 2102 | Nieciecza KS vs Legia Warszawa | 5.49 | 3.63 | 1.56 |
| 21:30 | 2990 | Fulham vs Brighton | 3.10 | 3.20 | 2.24 |
| 21:30 | 3033 | Peterborough vs Stevenage | 1.87 | 3.47 | 3.62 |
| 21:30 | 5396 | Crystal Palace vs Brentford | 2.08 | 3.34 | 3.34 |
| 21:45 | 1387 | Barnsley vs Lincoln | 2.14 | 3.29 | 3.04 |
| 21:45 | 1411 | Bordeaux vs US Quevilly Rouen | 1.98 | 3.20 | 3.80 |
| 21:45 | 1608 | Wigan vs West Bromwich | 3.39 | 3.24 | 2.10 |
| 21:45 | 1655 | Rangers vs Queen of South | 1.04 | 9.81 | 27.47 |
| 21:45 | 1939 | Annan Athletic vs Aberdeen | 14.72 | 6.87 | 1.13 |
| 21:45 | 2194 | Burnley vs Millwall | 1.69 | 3.49 | 4.99 |
| 21:45 | 2308 | Southampton vs Chelsea | 5.19 | 4.09 | 1.56 |
| 21:45 | 2432 | Roma vs Monza | 1.24 | 5.80 | 9.81 |
| 21:45 | 2672 | QPR vs Hull City | 1.90 | 3.41 | 3.86 |
| 21:45 | 3606 | Sheffield Utd vs Reading | 1.56 | 3.95 | 5.40 |
| 21:45 | 4467 | Cardiff vs Luton Town | 2.55 | 3.10 | 2.75 |
| 21:45 | 4724 | Ipswich vs Northampton | 1.68 | 3.58 | 4.41 |
| 21:45 | 5381 | Guingamp vs Sochaux | 2.54 | 3.04 | 2.79 |
| 21:45 | 5404 | Inter vs Cremonese | 1.13 | 7.77 | 15.94 |
| 21:45 | 5467 | St Etienne vs Bastia | 2.18 | 3.06 | 3.41 |
| 21:45 | 5683 | Birmingham vs Norwich City | 3.70 | 3.30 | 1.97 |
| 21:46 | 1782 | FC Teutonia 05 vs RB Leipzig | 35.74 | 17.36 | 1.03 |
| 22:00 | 1560 | Leeds vs Everton | 2.10 | 3.39 | 3.24 |
| 22:00 | 2175 | Watford vs Middlesbrough | 2.45 | 3.19 | 2.79 |
| 22:00 | 4276 | Rapid Bucuresti vs Universitatea Cluj | 1.84 | 3.19 | 4.49 |
| 22:15 | 2480 | Benfica vs Pacos Ferreira | 1.14 | 7.20 | 17.00 |
| 22:30 | 2791 | Zamalek vs Eastern Company SC | 1.29 | 5.25 | 9.08 |
| 22:30 | 3125 | Arab Contractors vs Al Masry Club | 1.82 | 3.11 | 4.92 |
| 22:30 | 3841 | Pyramids vs El Gouna | 1.53 | 4.02 | 5.83 |
| 22:30 | 5463 | Ghazl EL Mahallah vs El Ittihad Alexandria | 1.87 | 2.81 | 5.43 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# TPDC MARATHON KUSAIDIA WATOTO MATATIZO YA MOYO

**Na Gwamaka Alipipi**

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), limeandaa bonanza la mbio za marathon litakalojumuisha washiriki zaidi ya 500, lengo kuu likiwa ni kuwasaidia watoto wanaotarajiwa kufanyiwa upasuaji katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, JKCI.

Mbio hizo zitakazokuwa za urefu wa kilomita 21, kilomita 10, pamoja na kilomita tano, zimepewa jina la TPDC Marathon 2022 huku zikitarajiwa kufanyika Septemba 11, mwaka huu katika viwanja vya Farasi Oysterbay.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa TPDC, James Mataragio, alisema ni msimu wa kwanza kufanyika kwa mbio hizo na zitakuwa na kauli mbiu 'Kimbia kwa afya yako'.

"Tunawaalika Watanzania wote katika bonanza hilo, huduma zote za kimichezo zitakuwapo, pia tutashirikiana na Jeshi la Polisi kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwapo kwa washiriki," alisema Mataragio.

Aliongeza: "Tumekuwa tukishiriki katika kununua vifaa vya afya, huduma za michezo shuleni. Tumeona hiyo haitoshi tukaamua twende mbali zaidi tushiriki katika kuwasaidia watoto wanaohitaji upasuaji".

Alisema, fedha zitakazopatikana katika bonanza hilo zitakwenda kuwasaidia watoto zaidi ya 50 wenye matatizo ya moyo JKCI na kwamba mgeni rasmi atakuwa Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Profesa Mohamed Janabi, alisema watoto zaidi ya 500 wanasubiri kufanyiwa upasuaji JKCI, na gharama ya mtoto mmoja ni zaidi ya Sh. milioni nane.

Prof. Janabi alisema: "JKCI tunahudumia wagonjwa wengi kutoka nchi za jirani, upasuaji wa mgonjwa mmoja ni gharama kubwa sana. Kupitia marathon hii itakwenda kusaidia gharama hizo".

Alisema kwa mwaka zaidi ya watoto milioni mbili wanazaliwa Tanzania, kati ya hao asilimia moja (20,000), wanakuwa na tatizo la ugonjwa wa moyo, hivyo kila pesa itakayopatikana katika marathon hiyo itatutumika katika upasuaji wa watoto hao.

Aidha, aliwaomba Watanzania kujitokeza kushiriki katika marathon hiyo, sambamba na utoaji wa damu itakayosaidia kutumika katika upasuaji wa watoto hao.

**KIKAPU...**



Mchezaji wa Shule ya Sekondari Mtakuja (B), Ummy Anuary, akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa Sekondari ya Juhudi katika mchezo wa fainali wa michuano ya mpira wa Kikapu kwa Shule za Sekondari Mkoa wa Dar es Salaam, iliyomalizika juzi katika viwanja vya Don Bosco. Sekondari ya Juhudi ilitwaa ubingwa baada ya kushinda kwa vikapu 64-23. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kocha Azam wa kwanza kutimulia Ligi Kuu

**Na Adam Fungawango**

KOCHA Abdihamid Moallin wa Azam FC, amekuwa wa kwanza kutimuliwa kwenye Klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, ikiwa ndiyo kwanza ligi hiyo ipo raundi ya pili.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana, imesema imeafiki makubaliano ya kuachana na kocha huyo pamoja na Msaidizi wake, Omary Nasser kwa pande zote mbili.

"Tumefikia makubaliano ya pande mbili na kocha wetu, Abdihamid Moallin na Msaidizi wake, Omary Nasser, kuachia ngazi kama kocha mkuu na msaidizi mtawalia.

Hata hivyo, makocha hao wataendelea kubaki kama sehemu ya idara ya ufundi klabuni kwetu katika nafasi nyingine ambazo tutazitangaza hapo baadaye. Kwa sasa timu itakuwa chini ya Daniel Cadena, ambaye ni kocha wa makipa, hadi tutakapotangaza kocha mpya. Cadena ni kocha mwenye leseni ya juu kabisa ya ukocha, 'UEFA Pro License,'" iliandika klabu hiyo kwenye taarifa yake.


Alipotafutwa Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia maarufu kama 'Zaka Zakazi' ili kueleza sababu za msingi hasa zilizosababisha kuachana na makocha hao, ambao bado hawajafanya vibaya kwenye Ligi Kuu, simu yake ilikuwa ikiita bila kupokelewa kwa muda mrefu.

Kocha huyo ameondolewa kwenye nafasi yake, akitoka kulazimisha suluhu ya bila kufungana Jumamosi dhidi ya Taifa Jang'ombe kwenye mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

Kwenye mechi mbili za mwanzo, Azam imeshinda mchezo mmoja dhidi ya Kagera Sugar mabao 2-1 na kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Geita Gold, mechi zote zikipigwa nyumbani kwao, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Pia, anatimuliwa siku chache kabla ya mechi dhidi ya Mabingwa Watetezi, Yanga inayotarajiwa kupigwa Septemba 6, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Michezo
Jumanne Agosti 30, 2022
Nipashe



Xavi: Lewandowski ni kiongozi wa asili

# SIMBA YAPEWA FAILI LA BIG BULLETS CAF

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI juzi ikifanya vizuri kwenye mechi ya kirafiki ya kimataifa ya kujiwinda na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Klabu ya Simba imetamba kupata picha halisi ya kuanza kinyang'anyiro hicho wiki ijayo, lakini furaha zaidi ni baada ya faili zima la wapinzani wao, Nyasa Big Bullets kuanikwa.

Simba ambayo kwa sasa ipo nchini Sudan kwenye michuano maalum iliyoandaliwa na wenyeji wao, Klabu ya Al Hilal, kwa ajili ya kujiandaa na Ligi ya Mabingwa Afrika, juzi iliibuka na ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Asante Kotoko ya Ghana, shukrani kwa wafungaji Augustine Okrah, Pape Sakho na Clatous Chama aliyepachika mawili moja likiwa kwa njia ya mkwaju wa penalti.

Simba ambayo Septemba 10, mwaka huu, itashuka dimbani ugenini nchini Malawi kuivaa Nyasa Big Bullets kwenye mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kesho itashuka tena uwanjani kucheza mchezo wao wa mwisho wa kirafiki huko Sudan dhidi ya Al Hilal.

Akizungumza na gazeti hili jana, aliyekuwa mchezaji wa zamani wa timu ya Taifa ya Malawi na sasa ni kocha wa Kituo cha Soka la Vijana, (Walter Nyamilandu Football Academy) cha nchini Malawi, Joseph Kamwendo, amesema mabeki wa Simba wanatakiwa kuwa makini kuwachunga washambuliaji wa Big Bullets hususan Mnigeria Babatunde Adepoju, ambaye amekuwa mwiba mchungu kwa wapinzani wa Big Bullets kwenye Ligi Kuu ya Malawi.

Alisema amewafuatilia Simba na kubaini timu kubwa na ina wachezaji wenye majina makubwa, lakini anaamini mchezo huo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu ya timu zote zina vikosi bora.

"Safu ya ulinzi ya Simba inatakiwa kuwa makini zaidi kwa kucheza kwa nidhamu hali ya juu kwa kufuata maelekezo benchi la ufundi kwa sababu ya ubora wa safu ya ushambuliaji ya wapinzani wao hasa huyo Babatunde.

"Big Bullets wanasafu ya ulinzi imara, lakini hata Simba ina wachezaji wazuri na majina makubwa ninaamini itakuwa mechi ngumu na ya ushindani kwa sababu tayari Simba inafuatiliwa muda mrefu tangu walipomsajili Peter Banda," alisema Kamwendo.

Alisema baada ya CAF kutoa ratiba ya michuano hiyo na Big Bullets kupangwa kucheza dhidi ya Simba, wamekuwa wakiifuatilia zaidi hasa katika michezo ya ligi iliyocheza hivi karibuni na mchezo wa juzi dhidi ya Asante Kotoko nchini Sudan.

"Mara nyingi tumekuwa tukifuatilia zaidi mechi za Simba kwa sababu ya Banda ila baada ya CAF kutoa ratiba hiyo sasa inazidi kufuatiliwa kila mechi hasa benchi la ufundi la Big Bullets kuweza kuona ubora wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao," alisema nyota huyo wa zamani wa TP Mazembe.





Kiungo wa Simba, Clatous Chama, akipiga penalti iliyozaa bao la tatu dhidi ya Asante Kotoko ya Ghana wakati 'Wekundu wa Msimbazi' hao wakishinda mabao 4-2 kwenye mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyopigwa katika Uwanja wa Al Hilal nchini Sudan juzi. **PICHA: SIMBA**

Alisema mbali na Banda kutajwa, lakini kuna wachezaji wengine wa Simba ambao ni Pape Sakho (Ghana), Clotous Chama na Mosses Phiri (Zanbia) wamekuwa gumzo nchini Malawi lakini kutajwa ni wachezaji hatari na kutakiwa kuchungwa.

Wakati faili hilo la Big Bullets likianikwa, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amesema mechi ya juzi usiku dhidi ya Asante Kotoko imewapa picha ya michuano ya kimataifa wanayokwenda kucheza, akiwasifu wenyeji Al Hilal kwa kuwaalika kwenye mashindano hayo ambayo yanaonekana kuwajenga kuelekea kufanya makubwa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo juzi, Matola alisema: "Kwanza niwapongeze wachezaji, dakika tano za kwanza tulifanya makosa tukaadhibiwa, baadaye tukaikamata gemu na kupata nafasi nne za kufunga mabao, lakini tukatumia mbili, tungeweza kwenda mapumziko na mabao manne.

"Kipindi cha pili sisi tulishambulia na wao walikuja kwenye goli letu, lakini tuliweza kuwahimili na kuibuka na ushindi, kusema kweli tumepata faida kubwa kwenye mashindano haya, ni mazuri sana kwa sababu ndiyo kipimo halisi cha michuano ya kimataifa," alisema.

Matola alibainisha kuwa mechi hiyo imempa fursa Kocha Mkuu, Zoran Maki kuangalia wachezaji wengine ambao hakuwamo nchini Misri kwenye kambi ya kujiandaa na mwanzo wa msimu, lakini imewapa nafasi kuwaangalia wachezaji ambao hawakupata nafasi kwenye mechi mbalimbali ambazo timu hiyo imecheza.

## Kim atimuliwa Stars, Maxime, Kaseja ndani

**Na Adam Fungamwango**

SIKU moja tu baada ya Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kupata kipigo cha bao 1-0 nyumbani dhidi ya Uganda, kwenye mechi ya kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), Kocha Mkuu wa timu hiyo, Kim Poulsen amefungashiwa virago.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), na kusainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa shirikisho hilo, Cliford Ndimbo, imesema kuwa Poulsen na wasaidizi wake wamefikia makubaliano na TFF ya kuondoka kwenye timu hiyo ya taifa, lakini yeye ataendelea kuwa nchini katika timu za Taifa za Vijana mpaka mkataba wake utakapomalizika, nafasi yake ikichukuliwa na Hanour Janza ambaye ni Kocha Mkuu wa Namungo FC.

"Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limefikia makubaliano ya kumwondoa kocha wa timu ya Taifa, Taifa Stars, Kim Poulsen kwenye benchi la ufundi pamoja na wasaidizi wake.

"Pande zote mbili zimefikia makubaliano baada ya kikao cha pamoja. Paulsen ataendelea kubaki katika timu za Taifa za Vijana mpaka mkataba wake utakapomalizika.

"Kwa wakati huu benchi la ufundi la Taifa Stars litakuwa chini ya Kocha Hanour Janza akisaidiwa na Meck Maxime na kocha wa makipa, Juma Kaseja," ilisema taarifa hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >